


**Mwenyekiti,** Katibu wadaiwa 'kutwangana' makonde uchaguzi CCM

UKURASA 5



**SAMATTA AWAITA MASHABIKI KWA MKAPA**

UKURASA 23

Nipashe
Jumatatu Juni 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580968
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Mbowe: Nuru makubaliano

• **Ni** nia ya dhati ya Rais Samia utekelezaji... *Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### UKIINGIZA MIFUKO PLASTIKI FAINI MIL. 20/-

BARAZA la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), limesema mfanyabiashara atakayekamatwa akiingiza nchini vifungashio...

**UKURASA WA 3**

### IPP MEDIA KINARA USIMAMIZI MAZINGIRA

KAMPUNI ya IPP Media, imetangazwa kuwa kinara katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa hifadhi na usimamizi wa mazingira...

**UKURASA WA 5**

### WANAHISA NMB WAIDHINISHA GAWIO BIL. 96.7/-

WANAHISA Benki ya NMB wameidhinisha gawio la Sh. bilioni 96.7 kwa mwaka 2021, huku wakiwa...



## Maagizo 15 uhifadhi mazingira

UKURASA 3

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, yaliyofanyika Kitaifa kwenye ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma jana.
**PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**


## Wanafunzi 3 UDOM dereva Bajaji walivyofariki ajalini

UKURASA 2




**MICHEZO** NABI ATAKA REKODI YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alipokutana naye Ikulu. **PICHA: MAKTABA**

# Mbowe aona mwanga utekelezaji makubaliano

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema ameiona nia njema ya Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika kutekeleza makubaliano waliyoingia.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na Watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) kwa njia ya mtandao akiwaeleza masuala mbalimbali ya kitaifa pamoja na mipango ya chama chake.

Katika mkutano huo ambao ni wa kwanza kufanywa na Mbowe tangu atoke gerezani, aliwashukuru kwa mchango wao wa kumpigania wakati wote alipokuwa gerezani.

"Nitakuwa ni mnyimi kama nitasema Rais Samia hajaonyesha dhamira, Rais ameonyesha dhamira... amezungumza na mimi sio mara moja, ni mara kadhaa, na timu zote tulizokutana nazo katika Chama Cha Mapinduzi na hata hiyo kamati ndogo ya CCM na serikali yake ambayo tunakutana nayo sasa hivi, tayari watu wameonyesha commitment (utayari) ya hali ya juu katika kutekeleza yale ambayo tunafikiri tutakubaliana."

Mbowe alisema baada ya kikao cha mwisho kilichofanyika jijini Dodoma, alishakutana na Serikali ya CCM, ingawa haikutangazwa na anatarajia watakutana tena Juni 12, mwaka huu.

Alisema mazungumzo ya CHADEMA na Rais Samia yalilenga mambo makuu mawili ambayo ni namna ya kurejea katika mchakato wa kupatikana Katiba Mpya pamoja na mjadala mrefu wa safari ya kisiasa tangu mwaka 2016 hadi 2022.

"Hapa kuna mambo mengi ya kuangalia, kuminywa kwa siasa, sheria mbalimbali kandamizi, kesi za watu wetu mbalimbali ambao wengine wameshtakiwa na kufungwa. Watu wetu ambao wamepotezwa, watu waliopigwa risasi," alisema Mbowe.

**KIKOSI KAZI**

Hata hivyo, Mbowe alisema CHADEMA hakiungi mkono mwenendo wa kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, wakiamini kuwa tangu kilipoundwa kililenga kulinda maslahi ya watawala.

Alisema kikosi kazi hicho tangu kilipoundwa kilijipambanua kwamba hakihitaji Katiba Mpya kabla ya mwaka 2025, jambo ambalo linaenda kinyume na msimamo wa chama chao.

"Na sisi hatutohudhuria kwenye jukwaa lolote ambalo linakusudia kuahirisha mchakato wa Katiba Mpya mpaka uchaguzi wa 2025, katiba mpya ni sasa, na lazima tuijadili sasa," alisisitiza Mbowe.

Kadhalika, Mbowe alisema anataka katiba mpya yenye dhima ambayo itasaidia kubadilisha nchi, ikiwamo mfumo wa utawala wa nchi kutoka wa kijamaa wa kumtegemea kiongozi mmoja pekee kufanya maamuzi ya kila kitu.

"Ni wakati wa decentralize (kugatua madaraka), unakuta kuna waziri mmoja wa nishati, mdogo wangu January Makamba, kuna shida ya nishati, kuna shida ya petroli, kuna shida ya hiki basi January atafutwe, haiwezekani. Waziri mmoja wa elimu asimamie elimu ya nchi yote hii, haiwezekani," alifafanua.

Katika kuitafuta CHADEMA wanayoitaka, alisema kikao cha baraza kuu kilichopita wamepitisha mpango wa miaka mitano wa chama ambapo wamejikita katika mambo mawili ikiwamo kuweka mambo yao katika mfumo wa kidigitali ili kukua na teknolojia na kuwafikia wafuasi wengi kwa muda mfupi wakiwamo diaspora.

Akisema watajiunga na mfumo huo mapema mwezi huu (Juni) na kabla ya kufikia mwisho wa mwaka huu, asilimia 20 ya wapigakura wao waliopo Dar es Salaam wanajiunga katika mfumo wa kidigitali wa chama hicho.

**WALIOKIHAMA CHAMA**

Kuhusu viongozi walioondoka katika chama hicho, wakati wakiwa kwenye matatizo, Mbowe alisema hilo haliwazuii kuendelea na mapambano ya kukijenga chama chao.

"CHADEMA ina viongozi wengi kwenye matawi ikiwamo kwenye vyuo vikuu na diaspora ambao wanahitaji kuwatambua.

"Tunapofikiria kuitransform nchi (kuibadilisha) hatuwezi kufanya hivyo kama hatuna chama madhubuti. Lakini pili sio tu kwa kuwa na wanachana, bali wenye quality (sifa) za uongozi. Na quality sio u-profesa jamani, wala udaktari wala PHD...ila kuna suala la ethics (maadili), ambalo ni tatizo kubwa katika taifa."

"Kwa hiyo tunapojiandaa na uchaguzi mkuu ujao tunaanza kufikiria sasa hivi ni kina nani hasa wazuri kugombea ubunge. Tunawataka kina nani ambao tunafikiri wana uwezo mkubwa wa kugundua mambo ili watusaidie kujua kuunda serikali katika safari huko tunapokwenda."

Akizungumzia kelele za haki walizozipiga wanadiaspora hao kuwa yeye si gaidi wakati akiwa gerezani, alisema zilisaidia kwa kiasi kikubwa kulegeza mioyo ya walioishikilia kesi hiyo na hatimaye kuachiwa huru.

"Kwa hiyo napenda niwahakikishie wote kuwa mimi sio gaidi, sitokuwa gaidi na sijawahi kuwa gaidi, kwa hiyo kelele mlizopiga zilikuwa ni sahihi na haki kabisa," alisema Mbowe.

**MARIDHIANO**

Kuhusu maridhiano, alisema imekuwa ni sehemu ya uendeshaji wa chama hicho kwa miaka mingi, lakini serikali kwa muda mrefu haikutaka kwa sababu iliamini upinzani ni tishio.

Mbowe alisema baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, CHADEMA walikuwa na shauku ya kuzungumza naye, walimwandikia barua ya kuzungumza naye wakiamini kwamba wanahitaji kuwa na maridhiano.

Alisema alipotoka gerezani baada ya kuachiwa, hakusita kupokea wito wa Rais Samia alipomtaka kwenda kuzungumza naye Ikulu na anaona dhamira njema katika majadiliano ambayo wamekuwa wakifanya baina ya chama chake na CCM.

"Niseme wazi kwamba hadi wakati huu nimeona dhamira njema ya Rais Samia katika mazungumzo ambayo tumeyafanya na tutaendelea na mazungumzo hayo kwa awamu tofauti. Kama dhamira hiyo itaondoka basi hatutasita kujiondoa kwenye mazungumzo hayo," alisema.

Aliwataka wanachama wa CHADEMA kuwa wavumilivu wakati majadiliano hayo yanayoendelea huku akiwahakikishia kwamba kila kitu kitakwenda vizuri kwa maslahi ya chama chao.

## Wanafunzi 3 UDOM, dereva bajaji walivyofariki

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WATU wanne wakiwamo wanafunzi watatu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), wamefariki dunia na wengine watano kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha bajaji na gari ndogo aina ya RAV4 wakitokea kwenye mahafali ya dini chuoni hapo.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhusiano wa chuo hicho, Beatrice Baltazar, ajali hiyo ilitokea juzi saa 2:00 usiku katika moja ya barabara zilizopo chuoni hapo (block T), wakati wakirejea bwenini wakitoka kwenye sherehe ya dini ya kuwaaga wanafunzi wa mwaka wa tatu.

Akizungumza na Nipashe, Daktari wa Kitengo cha Dharura na Ajali katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, George Dilunga, alithibitisha kupokea miili ya marehemu hao pamoja na majeruhi watano.

Dk. Dilunga aliwataja waliofariki kuwa ni Fortunata Kiangazi (23), Anna Zilipenda (23), Melisa Mahenge (25) na dereva bajaji Peter Peter.

Aidha, aliwataja majeruhi kuwa ni Enika William, Asela Mey, ambao wapo kwenye chumba cha uangalizi maalum (ICU) huku Fide Julius, Sifa Shora na Furahini Fute, wakiendelea kupatiwa matibabu wodini.

Dk. Dilunga alisema majeruhi waliokuwapo kwenye gari aina RAV4 iliyogongana na bajaji hiyo ni Agnes William ambaye ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Alisema miili hiyo imehifadhiwa kwenye hospitali hiyo na majeruhi wanaendelea na matibabu.

Dk. Dilunga alisema: "Kwenye bajaji walikuwapo wanafunzi wanane na dereva bajaji, majeruhi watano wanafunzi wamelazwa katika hospitali hii."

## HABARI KITAIFA

# Kampuni ya IPP Media kinara usimamizi mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya IPP Media, imetangazwa kuwa kinara katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini na kupatiwa cheti na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Cheti hicho kilikabidhiwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika jijini hapa.

Pamoja na cheti hicho, pia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aligawa tuzo kwa mabalozi wa mazingira na viongozi wakuu watano ambao ni Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma.

Viongozi hao walipewa tuzo za heshima za mchango wao kwenye masuala ya mazingira.

Kadhalika, Mkoa wa Dar es Salaam umepatiwa tuzo ya usafi wa majiji, mkoa wa Iringa, Njombe na Katavi umepata tuzo ya kuendeleza uhifadhi, Mkoa wa Morogoro ukipata tuzo kwa kuongoza kampeni ya upandaji miti, huku Mkoa wa Dodoma ukipewa tuzo ya kampeni ya kukijanisha Dodoma.

Ilitolewa pia tuzo kwa wawakilishi 13 washindi wa kampeni kabambe kutoka kundi la mabalozi na wadau wa mazingira na vyombo mbalimbali vya habari vilipata vyeti vya kuelimisha umma masuala ya mazingira.

# Maagizo 15 uhifadhi mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amezindua mpango kabambe wa Hifadhi ya Mazingira nchini huku akitoa maagizo 15 ikiwamo kwa Wizara ya Fedha na Mipango, mpango huo kuwa sehemu ya vipaumbele vya bajeti vya kila mwaka.

Pia, amekemea tabia ya utiririshaji wa maji machafu kutoka viwandani na kwenye migodi ambao unachangia kuhatarisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana kwenye kilele cha Siku ya Mazingira Duniani kilichofanyika jijini hapa.

"Hivi karibuni tumeshuhudia kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai, maeneo mengi ya vyanzo vya maji yameathirika kutokana na ukame wa mara kwa mara, uchafuzi wa mazingira unaotokana na majitaka na kemikali kutokana na shughuli za viwandani. Uchafuzi huu umeendelea kuongezeka kwa kasi nchini na kuathiri maji, hewa na ardhi. Hali hii inahatarisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira."

Kuhusu mpango huo, aliitaka wizara hiyo kuwa sehemu ya vipaumbele vya bajeti vya kila mwaka kwa kipindi chote cha utekelezaji wake wa miaka 10.

"Wizara za kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe Mpango huu unajumuishwa katika mipango na bajeti zao, sambamba na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Ofisi ya Makamu wa Rais," alisema.

Aliagiza kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa maeneo yote yaliyoharibiwa yanarejeshwa kwa kupandwa miti, kila Mamlaka inatekeleza vema programu ya kitaifa ya upandaji miti milioni 1.5 ili nchi iwe ya kijani.

"Wizara, Taasisi, Mashirika ya Serikali na binafsi yanayotumia nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia au shughuli nyingine za uzalishaji zianze kutumia nishati mbadala, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ihakikishe matukio ya uchomaji ovyo misitu yanadhibitiwa," alisema.

"Kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka utaratibu wa kutenganisha taka na kukusanywa, mamlaka zinazohusika na usimamizi wa mifereji ya maji ya mvua mijini kusafisha mifereji hiyo ili kupunguza matukio ya mafuriko mijini," alisema.

Kadhalika, alitaka kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya misitu ya mijini katika mamlaka zao hayabadilishwi matumizi wala kuvamiwa.

Alizitaka sekta zinazohusika na usimamizi wa shughuli za umwagiliaji mashamba kuwa na matumizi sahihi ya maji yenye kuzingatia uhifadhi na ulinzi wa mazingira.

"Taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu zifanye tafiti kuhusu kuzuia na kudhibiti kuenea kwa viumbe vamizi vinavyochangia uharibifu wa mazingira nchini, mamlaka zinazohusika na usimamizi wa hifadhi za wanyamapori kudhibiti matukio ya ajali za barabarani kwa wanyamapori," alisema.

Taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu zifanye utafiti wa nishati mbadala ili kuondokana na utegemezi wa kuni na mkaa kwa kupikia.

Mamlaka zinazosimamia hifadhi za wanyamapori pamoja na mamlaka zingine kuzidhibiti shughuli za binadamu pamoja na uvamizi katika maeneo ya mapito ya wanyamapori (shoroba) ili kupunguza uharibifu wa mazao, mali na binadamu kupoteza maisha.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alisema ofisi yake imezindua mpango wa 'Soma na mti' ambao kila mwanafunzi anapaswa kupanda mti mmoja na wanafunzi milioni 14.5 kutoka shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu wameshiriki kwa kupanda mti mmoja mmoja.

Naye, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic, alisema vipaumbele vyao ni kuleta upatikanaji bora zaidi wa nishati na teknolojia jadidifu ili kusukuma ukuaji, kuwezesha usimamizi endelevu zaidi wa utajiri wa rasilimali za Tanzania.

**YALIYOMO KWENYE MPANGO**

Awali, akitoa maelezo kuhusu mpango huo, Mjumbe wa kikosi kazi cha kuandaa mpango huo, Thomas Bwana, alisema unaeleza matatizo yaliyopo ya mazingira na hatua ambazo zinapendekezwa kuzingatiwa ili kuondokana na athari za kimazingira.

Alisema kuna uharibifu wa ardhi, vyanzo vya maji, ardhi oevu, viumbe vamizi na kwa sasa hali sio nzuri shamba la Kongwa na eneo la Ngorongoro.

"Uharibifu wa ardhi upo sana maeneo ya Tabora, Singida, Shinyanga, mpango unaeleza hatua tunazokwenda kuchukua na sababu kubwa ni ukataji miti kwa shughuli za kibinadamu na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ambapo kwa kiwango kikubwa mkaa na kuni unatumika Dar es Salaam," alisema.

"Kuna ongezeko kubwa la mifugo ambapo imeonesha mifugo inahama kutoka maeneo ya Kaskazini kuja Kusini kwa mfano Mkoa wa Mtwara unaongezeko la takribani asilimia 700 ya mifugo kati ya mwaka 2008 hadi 2020."

Alisema kwa Mkoa wa Kigoma kuna ongezeko la takribani asilimia 800 ya mifugo na wametoa mapendekezo ya namna bora ya kufanya ufugaji usioharibu mazingira.

Kuhusu eneo la madini, mjumbe huyo alisema kuna ongezeko kubwa la upanuzi wa mashamba na mikoa mingi imeongeza mashamba hadi asilimia zaidi ya 1,200 kati ya mwaka 2008 hadi 2020.

Pia, alisema kuna ongezeko kubwa la mchanga kwenye maeneo ya mito, mabwawa, maziwa na baharini na eneo la Rufiji lina mchanga mwingi unaoingia baharini na kuchangia kuharibu ikolojia.

"Kwenye ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere tusipodhibiti sehemu kubwa ya mchanga itaendelea kubaki kwenye bwawa lile. Tumeonesha katika eneo la mtiririko wa maji eneo kubwa la mabonde Kusini kwenye Ziwa Rukwa, Nyasa kuna upungufu mkubwa wa maji kwa miaka hiyo 10, pia Ziwa Victoria limeendelea kupungua maji, unafuu upo kwenye mabonde ya kati, tunapendekeza hatua mbalimbali ili kuondoa hali hii," alisema.

Kuhusu usimamizi wa taka, alisema zinazalishwa nyingi kuliko zinazokusanywa na maeneo mengi yanapokea taka kwa asilimia 35 kuliko inavyokusanya.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya SINGIDA

Kituo cha NONGERO Mkoa SINGIDA

Shauri la Ndoa Na. 4 /2022

Jina la mdai.......................................HAMIDA HAMISI HASSAN

Jina la mdaiwa..........ABRAHAMAN HUSEIN AMAN WA ZANZIBAR

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za mwanzo)

Kwa ABRAHAMANI HUSSEN AMANI
KK. HAKIMU MFAWIDHI MAHAKAMA YA WILAYA

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba( eleza hapa habari za madai)

**TALAKA(KUACHANA) MGAO LA CHUMO LA PAMOJA.** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15 mwezi06 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 05 mwaka 2022

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
ILONGERO

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO 163 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late MGESI ZAKARIA MACHANGO**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**DAVID ZAKARIA MACHANGO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 5th day of **July, 2022.**

**Dated at DAR ES SALAAM this 03 day of 06, 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate


## KUPOTEA KWA CHETI



**JUMA JOSEPH SILAS** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha Chuo chenye namba **03.5782.01.01.2014** kilichotolewa na **COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION** mwaka 2019. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI: **DAR/MSI/RB/188636/2022.**

## INVITATION FOR BIDS

SGS

| | REF NUMBER | REG # | TYPE | MAKE & MODEL | YOM | LOCATION | CONTACT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TZ_VEH0000085 | MC812BER | MOTOR CYCLE | BAJAJ BOXER BM150 (Red) | 2016 | Dar es salaam -SGS Office, Kinondoni | Anna Moshy - 0756454968 |
| 2 | TZ_VEH0000084 | MC913BEN | MOTOR CYCLE | BAJAJ BOXER BM150 (Red) | 2016 | | |
| 3 | TZ_VEH0000078 | T997DFR | MOTOR VEHICLE | TOYOTA RAV4 (COLOR BLACK) | 2005 | | |
| 4 | TZ_AA/VEH0015 | T724AEY | MOTOR VEHICLE | MITSUBISHI PICK UP, DC, 4X4 | 2003 | Mwanza -SGS Office, Mkuyuni | Alex Nairo - 0755754882 |
| 5 | TZ_AA/VEH0042 | T609APK | MOTOR VEHICLE | MITSUBISHI FUSO TRUCK | 1995 | | |
| 6 | TZ_AA/VEH0045 | - | CRANE | TRUCK CRANE | - | | |
| 7 | TZ_AA/VEH00XX | - | FORK LIFT | FIAT FORK LIFT | - | | |

Vehicles are sold on "AS IS WHERE IS BASIS" and viewing can be done at various locations indicated above during normal working hours **10:00 AM to 16:00 PM from 8th June to 16th June 2022.** Interested bidders must pay a non-refundable fee by Depositing TZS. 25,000 ECO Bank a/c # 7945002612 and submit the slip attached with your bid in our tender boxes located at the reception for Dar es salaam and Mwanza. Bids should be submitted, not later than **18th June, 2022 by 10.00 AM.**

**For more details please contact us via +255 756454968 for Dar es salaam / 0755 755754882 for Mwanza or alternatively e-mail us at TZ.Procurement@sgs.com**

WWW.SGS.COM WHEN YOU NEED TO BE



Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Kilimo na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi Kilele ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda, Viungo na Mazao yatokanayo na Mizizi (TAHA), Dk. Jacquiline Mkindi (aliyevaa koti jeusi), akikagua baadhi ya bidhaa zilizozalishwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi jana, alipokwenda kufungua tamasha la ubunifu na vipaji. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Ukiingiza mifuko plastiki faini mil. 20/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), limesema mfanyabiashara atakayekamatwa akiingiza nchini vifungashio vya mifuko ya plastiki atatozwa faini ya Sh. milioni 20.

Pia, muuza duka au genge atakayekutwa na vifungashio hivyo atatozwa faini ya Sh. 30,000 au kifungo cha siku saba.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira kutoka NEMC, Redempta Samwel, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa maofisa mazingira wa wilaya na Mkoa wa Dodoma.

"Kosa la kuingiza nchini mifuko ya plastiki ni kuanzia Sh. milioni 20 au kifungo cha miaka saba au vyote kwa pamoja, lakini kuna makosa ya wewe mwananchi wa kawaida ambaye ni mama una genge lako sokoni unakutwa na ile mifuko mingi imewekwa ili mteja awekewe bidhaa, ukikamatwa faini yake ni Sh. 30,000 au kifungo cha siku saba au vyote kwa pamoja."

Alisema serikali ilishachukua hatua ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kwa sasa mifuko ya rambo haipo isipokuwa kuna tatizo limeibuka la matumizi mabaya ya vifungashio.

"Kanuni ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki iliruhusu baadhi ya matumizi ambayo ni kwa ajili ya kuhifadhi ubora wa vitu, ubora wa bidhaa kwenye viwanda sekta ya kilimo na kwingine, lakini kumetokea matumizi mabaya ya vifungashio, jamii imegeuza vifungashio kuwa vibebeo, kifungashio kinatakiwa kufungasha bidhaa kabla ya kupeleka sokoni," alisema.

Alisema maofisa mazingira ndiyo wasimamizi wa utekelezaji wa sheria ya mazingira kwenye maeneo yao na wamepewa elimu ya kutambua vifungashio ambavyo vimeruhusiwa na visivyoruhusiwa. "Kifungashio hakitakiwi kuwapo sokoni, kinachotakiwa ni bidhaa iliyofungashwa, kwa hiyo mwananchi au mteja yeyote anayekwenda dukani kununua kitu, anapowekewa kwenye mfuko wa plastiki ni kosa kisheria kwa kuwa kimetumika kama kibebeo hakijafungasha bidhaa," alisema. Aliwasihi wananchi kujiepusha na matumizi ya mifuko hiyo inayochafua mazingira kwa kutumia mifuko mbadala huku akishauri waende na vikapu sokoni.

"Tumeshuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na mifuko ya plastiki, ndiyo maana serikali imekataza matumizi yake. Baraza pamoja na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa katazo la mifuko hii tunafanya ukaguzi, serikali haijalala, tunajua kuna uingizaji wa mifuko kutoka nchi za jirani kinyemela," alisema na kuongeza.

Akifungua mkutano huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameagiza Baraza hilo kudhibiti hali hiyo kwa kusimamia sheria na taratibu zilizopo kwa kuwa ni kosa kisheria.

"Kwa kiwango kikubwa tumefanya kazi nzuri katika kudhibiti mifuko ya plastiki, lakini sasa tunachangamoto ya vifungashio ambavyo watu wamegeuza kuwa vibebeo, nendeni mkasimamie sheria katika hilo. Pia nitoe rai kwa wawekezaji kuendelea kuzalisha mifuko mbadala."

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema tatizo lililopo ni kutosoma Sheria ya mwaka 2004 na kanuni zake ambazo zimetoa mamlaka makubwa kwa maofisa mazingira kusimamia kwenye maeneo yao.

## Madereva bodaboda wampa 5 Samia kushuka bei ya mafuta

**Na Boniface Gideon,** TANGA

UMOJA wa Wamiliki na Waendesha Pikipiki Wilaya ya Tanga (UWAPIBATA), wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua ya kusimamia bei ya mafuta kushuka.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, kwenye kikao kilichoshirikisha madereva pikipiki na Jeshi la Polisi, Mwenyekiti wa UWAPIBATA, Mohamed Chande, alisema wanaipongeza serikali kwa hatua ya kushusha bei ya mafuta na Rais Samia kwa kuwa imewapa unafuu katika kazi zao.

"Kitendo cha serikali kupitia Rais Samia na kwa kuzingatia kuwa nchi za wenzetu zimekumbwa na uhaba mkubwa wa mafuta na kusababisha foleni, sisi kama UWAPIBATA tunampongeza Rais Samia kwa kutoa ruzuku hii ambayo imesaidia kupunguza makali ya bei ya mafuta kwa Watanzania," alisema Chande.

Chande alisema kabla ya ruzuku walikuwa wakinunua mafuta aina ya petroli kwa Sh. 3,137 kwa lita, lakini kwa sasa bei ya mafuta hayo inauzwa kwa Sh. 2,985.

Alisema mafuta aina ya dizeli awali ilikuwa yanauzwa kwa Sh. 3,639, lakini kwa sasa hivi ni Sh. 3,162.

"Tunatoa wito kwa serikali yetu ichukue hatua zaidi za kikodi kwenye Bajeti Kuu ya Serikali kupitia Bunge letu linaloendelea jijini Dodoma, lengo letu tunataka bei za mafuta zishuke zaidi ya hapa kuanzia mwaka mpya wa fedha 2022/2023, hii itasaidia kupunguza makali ya mfumuko wa bei na gharama za maisha kwa wananchi," alisema Chande.

EWURA ilitoa maelekezo ya bei mpya za mafuta ya petroli na dizeli nchini, kwa Mkoa wa Tanga petroli ilishuka kwa Sh. 152 kwa lita moja huku dizeli pia ikishuka kwa Sh. 152 kwa lita moja.

# Mbarawa: TANROAD mjitathmini malalamiko ya madereva mizani

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amewataka watendaji wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROAD), wanaofanyakazi kwenye mizani ya kupima uzito wa magari, kujitathmini katika utendaji wao kutokana na malalamiko ya wamiliki wa magari kutotendewa haki kwenye mizani. Alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa mizani mipya ya kisasa iliyopo eneo la Kimokouwa Wilaya ya Longido, iliyojengwa kwa fedha za ndani kwa asilimia 100 na kugharimu Sh. billion 14.718.

"Najiuliza kwanini mizani A ikipima inapata tani 10, lakini gari hili hili likifika mizani B anaambiwa ni tani 11 au zaidi, kwanini, naomba mjitafakari malalamiko ni mengi, madereva wananipigia simu kila leo wakilalamika," alisema.

Aidha, alisema kumekuwapo na watendaji wachache wa TANROAD wanaojihusisha na masuala ya rushwa katika utendaji kazi na hali hiyo husababisha kuwaandikia faini waliozidisha mzigo baada ya kushindwa kukubaliana kama ilivyo matarajio yake.

"Unakuta Mtendaji kaomba rushwa laki moja yule mtu hana, hivyo anapakiwa pembeni na kuandikiwa faini, ukiletewa ile faini ukitizama na thamani ya gari unakuta gari ina thamani ya Sh. milion 10, lakini faini aliyoandikiwa ni Sh.milioni 30 ataitoa wapi?" Alihoji. Katika hatua nyingine aliwataka wamiliki wa magari kuzingatia sheria za nchi ikiwamo za barabara kuepuka kuzidisha mizigo kwenye magari ili kuepuka faini zisizo za lazima.

Alisema katika kuzingatia utunzaji wa miundombinu ya barabara, serikali imejenga vituo vya kupimia uzito wa mizigo iliyobebwa kwenye magari lengo likiwa ni kudhibiti uharibifu wa barabara na kupunguza ukarabati wa mara kwa mara ambao huongeza gharama.

Mkuu wa wilaya hiyo, Nurdin Babu, aliiomba wizara hiyo kufunga taa maalum za barabarani kuanzia mpaka wa Namanga hadi makao makuu ya wilaya hiyo kutokana na barabara hiyo kupita watalii kutoka mataifa mbalimbali.

Naye mbunge wa jimbo hilo ambaye pia ni Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alimshukuru Rais Samia kwa kujenga kituo cha kupimia uzito wa magari na kuiomba wizara kumalizia ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 44 kwa kiwango cha lami.

Mwakilishi wa wazee wa kimila wilayani hapa (Alaigwanani), Thomas Ole Ngulipa, aliomba serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwa wazawa wa wilaya hiyo hususani kutoka katika kata ya Kimokouwa kutokana na wananchi kutoa eneo la ujenzi ili wanufaike na mradi huo.

Mtendaji Mkuu wa TANROAD, Mhandisi Rogatus Mativila, alisema mradi huo umejengwa kwa fedha za ndani Sh. bilioni 14, lakini tatizo lililopo ni wafugaji kuingiza mifugo katika eneo la mizani pamoja na uharibifu wa alama za barabarani.

"Mradi huu uliwanufaisha wananchi kwa ajira za kudumu na za muda mfupi, Watanzania 270 walipata ajira huku wageni wakiwa 12 pekee, lakini pia mamalishe walinufaika kwa kuuza vyakula," alisema Mhandisi Mativila.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongela, alisema Wilaya ya Longido ni ya kimkakati katika mkoa wake kutokana na kuwa eneo la uwekezaji na vyote vinavyofanyika ikiwamo miradi ya maendeleo vinaongeza thamani ya mkoa huo.

HABARI KITAIFA

# Mwenyekiti, Katibu wadaiwa 'kutwangana'

Na Richard Makore, MWANZA

KATIKA hali ya kushangaza, Mwenyekiti wa Wilaya ya Musoma, Magiri Benedictor na Katibu wa Wazazi wilaya hiyo, Zainab David, wanadaiwa kupigana ngumi wakati wa uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tawi la Nyasho Kati.

Ugomvi huo ulisababisha uchaguzi uliokuwa ukifanyika kuahirishwa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Katibu wa Wilaya ya Musoma, Burhan Ruta, alikiri kutokea kwa mtafaruku huo na kuamua kuahirisha uchaguzi huo.

Taarifa zilizoifikia Nipashe zinadai kuwa kwenye kikao hicho Mwenyekiti huyo alitinga kwenye kikao hicho na kutaka kushinikiza mgombea wake apitishwe bila kufuata kanuni za uchaguzi.

Ruta alisema kanuni za uchaguzi katika chama hicho zipo wazi na kwamba yeye ndiye amepewa jukumu la kuzisimamia na kuhakikisha uchaguzi unafanyika katika ngazi zote za wilaya.

"Mimi ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ngazi zote ndani ya CCM, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, nitahakikisha hakuna kanuni inayokiukwa," alisisitiza.

Alikiri katika uchaguzi huo uliokuwa ukifanyika katika Tawi la Nyasho Kati kwamba alipofika Mwenyekiti wake, zilitokea fujo na kumfanya aahirishe kikao, ingawa hakutaka kuzungumzia iwapo Mwenyekiti huyo alimrushia ngumi katibu wake wa wazazi.

Ruta alisema atahakikisha anasimamia kanuni na miongozo mbalimbali katika uchaguzi na hatakubali kuyumbishwa na mtu yeyote.

"Sisi tulioteuliwa na vikao halali vya chama tutahakikisha kanuni zote zinazoongoza uchaguzi huu zinafuatwa bila kumuogopa mtu yeyote ama kumuonea," alisema.

Mmoja wa makada walioshiriki uchaguzi huo (jina limehifadhiwa), alisema siku ya uchaguzi, Mwenyekiti alitaka kushinikiza mgombea wa nafasi ya mwenyekiti apitishwe bila kupigiwa kura kwa madai kuwa alikuwa hana upinzani.

Alisema kanuni zinataka mgombea hata kama yupo peke yake lazima apigiwe kura za ndiyo ama hapana na wajumbe wote wenye sifa za kupiga kura, jambo ambalo linadaiwa kukataliwa na mwenyekiti huyo.

Kada huyo alidai kuwa kilicholeta shida ni viongozi kutaka kupanga safu ya uongozi ndani ya chama hicho, ili wawasaidie watakapogombea nafasi mbalimbali miezi mitatu ijayo.

Akizungumzia madai hayo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma, Magiri Benedictor alikana kuhusika na vurugu katika uchaguzi huo.

Benedictor alisema kilichosababisha kuahirishwa uchaguzi ni mgombea kutokuwa na kadi, kuwapo wanachama wasiokuwa na sifa pamoja na kuchakachuliwa karatasi za kupiga kura.

Pia, alikana kumrushia makonde Katibu wake kwa madai kuwa yeye ni mtu mzima na hawezi kufanya jambo hilo.

Alipoulizwa ilikuwaje yeye kushiriki uchaguzi wa tawi ambao haumhusu, Benesictor alisema ni kiongozi wa chama ngazi ya wilaya na anaweza kwenda sehemu yoyote anapobaini mambo hayaendi sawa.

Katibu wa Wazazi Wilaya ya Musoma, Zainabu David, alikiri kutokea vurugu katika uchaguzi huo baada ya yeye kumsomea Mwenyekitii kanuni zinazosimamia uchaguzi huo.

Alisema wakati akisoma kanuni hizo wanachama wanatakiwa kumpigia kura za ndiyo ama hapana mgombea ambaye yupo peke yake, ndipo mwenyekiti huyo alipomvamia na kuanza kumshambulia na kusababisha Katibu aahirishe uchaguzi huo.

Diwani wa Viti Maalum wilayani humo, Naima Minga, alisema hiyo ni mara ya pili uchaguzi huo kuahirishwa katika tawi hilo kutokana na vurugu.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, CPA Innocent Rwetabura (kulia) akiongea wakati wa uzinduzi wa mkakati wa usajili wa uzazi kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano mkoani Tabora mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanahisa NMB waidhinisha gawio Bil. 96.7/-

Na Mwandishi Wetu

WANAHISA wa Benki ya NMB wameidhinisha gawio la Sh. bilioni 96.7 kwa mwaka 2021, huku wakiwa na imani benki kufanya vizuri zaidi. Gawio hilo linatokana na kuongezeka kwa faida baada ya kodi kuongezeka kutoka Sh. bilioni 206 mwaka 2020 na kufikia Sh. bilioni 290 mwaka 2021.

Katika mkutano mkuu wa 22 wa mwaka uliofanyika mwishoni mwa wiki, wanahisa walipitisha kiasi hicho cha fedha ambacho ni sawa na malipo ya Sh. 193 kwa kila hisa kwa kipindi kilichoishia Desemba 31, 2021.

Akizungumza na wandishi wa habari baada ya mkutano huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema benki hiyo itaendelea kuvuka malengo iliyojiwekea kwa mwaka huu pia.

Matarajio hayo yanatokana na matokeo mazuri ya robo ya kwanza ya mwaka huu na tayari imepata faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 101 ikiwa ni ongezeko la asilimia 55 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

"Mafanikio makubwa ya kiutendaji kwa mwaka 2021 na matokeo mazuri ya robo ya kwanza ya mwaka 2022 ni kielelezo cha ufanisi mzuri unaotokana na utekelezaji makini wa mikakati yetu. Tutaendelea kutekeleza kwa umakini sana mikakati tuliyojiwekea na tunaamini kwamba malengo tuliyojiwekea kama benki tutayafikia na kuyapita mwaka huu wa 2022," alisema Zaipuna.

Alisema kwa mahesabu ya kawaida, matokeo ya robo ya kwanza ya mwaka huu yanaleta picha kuwa utakuwa mwaka mzuri pamoja na changamoto zinazoendelea kujitokeza duniani.

## TARI kusambazia mawakala tani 80 za mbegu

Na Renatha Msungu

KITUO cha Utafiti wa Mbegu (TARI) Ilonga, kinatarajia kuzalisha tani 80 za mbegu aina TARI-ILO na TARI-NA na kuzisambaza kwa mawakala wa mbegu na wakulima mikoani kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk. Lameck Makoye, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mbegu aina ya TARI-ILO na TARI-NA ambazo zimefanyiwa utafiti na watafiti wa kituo hicho. Dk. Makoye alisema wamepanga kuzalisha mbegu hizo ili kuzitawanya katika maeneo mbalimbali ya wakulima kwa lengo la kutumika kwa wingi msimu ujao wa kilimo. Alisema katika tani ambazo wamepanga kuzalisha msimu ujao, 40 zitapelekwa kwa Wakala wa Usambazaji Mbegu nchini (ASA), zitakazosalia zitagawiwa kwa wakulima kupitia vituo vya utafiti vilivyopo katika kanda mbalimbali hapa nchini.

"Tumejipanga kuzalisha tani 80 za mbegu aina ya TARI-ILO na TARI -NA. Tunahitaji kuona zinapatikana kwa wingi ili wakulima wote wazitumie lengo ikiwa ni kukabiliana na upungufu wa mafuta nchini, lakini pia kuongeza uzalishaji," alisema Dk. Makoye.

Alisema pia mbegu hizo zina ubora wa kutosha ikiwamo kuwa na ustahimilivu wa wadudu waharibifu wa zao hilo endapo watatokea kipindi cha kupanda.

Kuhusu uzalishaji wa alizeti, alisema watahakikisha wanafanya utafiti kwenye mbegu ili waweze kugundua zinazostahimili mazingira ya Tanzania.

Alisema TARI Ilonga ipo kwa ajili ya kufanya utafiti wa mbegu bora ili kuwasaidia wasambazaji wa mbegu kusambaza mbegu bora kwa wakulima katika mikoa mbalimbali, nchini.

Mratibu wa alizeti nchini, Mtafiti Frank Reuben alisema mbegu aina ya TARI-ILO na TARI-NA zinafaida kwa wakulima endapo watazitumia vizuri kwa kufuata maelekezo kutoka kwa wataalamu.

Alisema moja ya faida ya mbegu hizo ni zinakinzana na wadudu waharibifu wa zao hilo, zinatoa mavuno mengi pindi msimu wa mavuno utakapokaribia na hutoa mafuta mengi.

Reuben alisema wakulima wanapaswa kuchangamkia mbegu hizo ili waweze kuzitumia katika msimu ujao wa kilimo.

Aliwataka wakulima kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalam na watafiti wa kilimo wanapokuja kutoa elimu kwao.

Alisema TARI Ilonga imejipanga kuhakikisha mbegu ambazo zimefanyiwa utafiti zinawafikia wakulima kwa wakati ili waweze kuzitumia kwa wingi katika msimu ujao wa kilimo cha alizeti.

water mission TANZANIA

Water Mission Tanzania imedhamiria kutekeleza mpango wa miradi katika eneo la Kigoma na Dodoma, kwa lengo la kuhudumia jamii na taasisi zenye uhitaji wa huduma ya maji safi na salama katika nchi mwenyeji ya Tanzania. Tunapenda kukualika kuhudhuria kikao cha wadau wote kitakachofanyika tarehe na mahali tajwa katika kila mkoa. Tafadhali wasiliana na Water Mission Tanzania kwa njia ya baruapepe **WMT@watermission.org** au kwa WhatsApp namba **0748207781** kwa maelezo zaidi. Unaweza pia kushiriki kikao hiki kwa njia ya mtandao kwa kujiunga na anwani/kiunganishi kifuatacho kwa tarehe/saa na mahali tajwa:

Kigoma: Saa 3:00 asubui 6 Julai Mahali: Upendo Lodge, Kasulu Mjini. Join online at:

**https://watermission.zoom.us/j/86420036796?pwd=NWFoVlRDVFQxbXBVSFY0OmlLeTVpdz09**

Dodoma: Saa 4:00 asubui 13 Julai Mahali: Kilimo Hall, Chamwino Wilayani. Join online at:

**https://watermission.zoom.us/j/83439556772?pwd=TGVuQ0VuY3pza3FKY3VMTUYyL2hXZz09**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF nendeni na ratiba CAF, Simba, Yanga mulikeni usajili

**MSIMU** wa Ligi Kuu Bara 2021/22, umebaki raundi nne kwa kila timu kabla ya kumalizika ifikapo Juni 29, mwaka huu, ambapo klabu zote 16 shiriki zitakuwa zimecheza mechi 30 kila moja na baada ya hapo ndipo dirisha rasmi la usajili kuelekea msimu mpya litafunguliwa.

Kumalizika kwa msimu pia, huwezesha kujulikana kwa timu zitakazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF; yaani Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Kama ilivyokuwa msimu uliopita, ujao pia Tanzania imepata nafasi ya kuwakilishwa na timu nne, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Ikumbukwe pia bingwa wa Ligi Kuu na mshindi wa pili, ndio hubeba dhamana ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati timu itakayoshika nafasi ya tatu na ile itakayotwaa Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup), ndizo hukata tiketi ya kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hivyo, wakati Ligi Kuu ikitarajiwa kumalizika Juni 29 huku fainali ya Kombe la FA ikitarajiwa kuchezwa Julai 2, mwaka huu, michuano ambayo itatoa wawakilishi wetu wa nchi kimataifa, tayari CAF imepuliza kipenga cha siku ya kufungwa kwa dirisha lake la usajili wa wachezaji na klabu zitakazoshiriki michuano yake hiyo miwili.

Kwa mujibu wa taarifa ya CAF, dirisha hilo litafungwa Juni 30, mwaka huu siku moja baada ya kumalizika Ligi Kuu Bara na siku tatu kabla ya fainali ya Kombe la FA nchini, ambalo hutoa mwakilishi wetu kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hivyo, kutokana na Kalenda ya TFF, hadi tarehe hiyo ya kufungwa kwa dirisha la usajili la CAF, itakuwa haijajulikana mwakilishi wa nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwani fainali ya FA Cup kati ya Yanga na Coastal Union itapigwa Julai 2, jambo ambalo linahitaji marekebisho ya haraka ili kuendana na kalenda hiyo.

Ni wazi presha kubwa itakuwa kwa upande wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, kwani Yanga ambayo inacheza fainali ya FA, tayari ina tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa sambamba na Klabu ya Simba.

Yanga hadi sasa ina pointi 64 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu huku ikifuatiwa na Simba yenye alama 51, pointi ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote katika ligi hiyo kwa sasa, kwa maana hiyo vigogo hivyo vya nchi moja kwa moja vina tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Kinachotakiwa kwao kwa sasa ni kuanza kuingia makubaliano na wachezaji wanaotaka kuwasajili na kusaini mikataba ya awali baada ya pande zote kukubaliana ili ligi tu itakapokamilika kukamilisha mchakato huo wa usajili na kuwahi kuwasilisha majina ya nyota wao CAF kabla ya dirisha kufungwa.

Lakini pia ni wakati wa TFF na Bodi ya Ligi kujichimbia na kufanya marekebisho ya ratiba haraka ili Ligi Kuu imalizike katikati ya mwezi huu kuwezesha wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya CAF kujulikana pamoja na dirisha la usajili kufunguliwa mara moja.

Kadhalika, hatuoni sababu ya fainali ya FA kupigwa Julai 2, wakati inaweza kufanyika mapema hata kabla ya Ligi Kuu kumalizika ili kutoa nafasi kwa mshindi kujipanga kwa michuano hiyo ya CAF hasa ukizingatia timu ambazo hupata nafasi hiyo nyingi husumbuliwa na ugeni wa mashindano hayo pamoja na uwezo kiuchumi.

Tunatambua baada ya dirisha hilo la CAF kufungwa hutolewa wiki mbili kwa klabu kuomba kufunguliwa kufanya usajili lakini kwa kulipia, hivyo kama timu hazitafanya usajili wao mapema, ikiwa ni pamoja na TFF kuhakikisha ligi inamalizika mapema zaidi, kutazigharimu sana klabu zetu ambazo baadhi kiuchumi hazipo vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaohoji bil. 20/- za Mo hawaiamini serikali?

**MARA** baada ya Simba kushindwa kuutetea ubingwa wake na kufungwa na Yanga kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, kumezuka sintofahamu kutoka kwa waliokuwa viongozi wa zamani wa klabu hiyo.

Viongozi hao ambao kwa nyakati tofauti, ingawa hazizidi wiki moja, wamekuwa wakiongea maneno ambayo yanaonekana kuwa hali si shwari ndani ya klabu hiyo.

Wengine ni Wajumbe wa Bodi ambao wanakwenda kwenye redio na kuongea vitu ambavyo ilibidi waviongee kwenye vikao vyao. Inawezekana kuwa ni kweli kuna tatizo kwa baadhi ya viongozi, lakini kinachotia shaka ni kwamba kwa nini viongozi wote waongee wakati huu?

Ni kwa nini waongee mara baada ya timu kufanya vibaya? Ni jinsi ambavyo kila mmoja alikuwa akilaumu kivyake, inaonekana ni kwamba matatizo hayo yapo kwa muda mrefu.

Cha kujiuliza ni kwa nini siku zote hizo wasiongee? Kama kuna tatizo kwa baadhi ya watendaji, nadhani ingekuwa vizuri wao kuongea hata pale ambapo timu inafanya vizuri.

Hii ingewaletea kuaminika, lakini hata kama ni kweli, kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba wanashindwa kuwaelewa kwa sababu muda ambao wameutumia kulalamika si sahihi. Wengi wanaona kwamba kitendo cha kutoongea kwenye bodi, badala yake kwenda kwenye vyombo vya habari, tena wakati huu ambao Simba imekosa ubingwa na Kombe la FA, ni nia ovu ya kutengeneza mgogoro.

Hata kama waliona kwenye vikao hawasikilizwi, je baada ya kusikika kwenye vyombo vya habari ndiyo watatekeleza?

Kinachoshangaza ni muda mfupi wa viongozi hao wote kulizungumzia jambo hilo. Hata mzee Hamisi Kilomoni naye ameongea kuhusu kuwashutumu baadhi ya watendaji Simba kwenye kipindi hiki hiki kifupi kisichopungua wiki moja tu. Mpaka baadhi ya watu wanadhani labda waliambizana.

Lakini wapo wanaodhani kuwa haya yote pia huenda yanaletwa na kuwapo kwa uchaguzi baadaye mwaka huu. Yaani watu wameanza kampeni.

Kwa bahati nzuri, wanachama na mashabiki wa sasa siyo wale ambao walikuwa wakiwaongoza wao wakati huo. Hawa ni wapenda maendeleo zaidi na si wachumia tumbo, waliokuwa wanashinda klabuni kuomba pesa kwa viongozi, na hawapo kwa maslahi ya timu, hivyo kuanza kuzusha mgogoro.

Hawa wa sasa wengi wana kazi zao, wanaichangia mpaka klabu pesa zao wenyewe, wapo kwa ajili ya maendeleo na klabu kupata ushindi.

Kingine ninachoshangaa ni baadhi ya watu, wadau na viongozi kuulizia pesa za Rais wa Heshima na Mwekezaji, Dk. Mohamed 'Mo' Dewji kuwa ziko wapi na kama zipo zimewekwa benki gani?

Awali, nilidhani swali hili limekaa kiutani zaidi kwa mashabiki wa watani zao wa jadi, ili kurushana roho, lakini inaonekana mpaka baadhi ya watu wa Simba na hata wachambuzi wameanza kuhoji hilo.

Nchini England, bilionea Todd Boehly ameinunua klabu ya Chelsea kwa paundi bilioni 4.25 kutoka kwa mmiliki wa awali Romam Abramovic, hatujasikia mchambuzi yeyote wa England, Ulaya, au hata hapa hapa Tanzania kuhoji hizo pesa zimewekwa benki gani.

Hayo ni mambo ya kibiashara yanawahusu wafanyabiashara, huku serikali ya England ikiwa imesimamia mchakato wote. Ina maana watu wanaiamini serikali.

Hapa kila kukicha kuna watu wanauliza pesa ya Mo imewekwa benki gani, kweli tuko makini au ni utani? Hivi wanaouliza wanaweza wao wakatuambia pesa zao wameweka benki gani?

Halafu hivi mtu kama Mo, mfanyabiashara mkubwa duniani, aongope kuweka pesa? Nakumbuka Julai 30, mwaka jana ndipo alipoweka kukawa na hafla ambayo serikali nayo ilihudhuria kupitia kwa Tume ya Ushindani ya Biashara ambayo nakumbuka ilikaa muda mrefu ikitaka warekebishe mambo kadhaa na baada ya kujiridhisha wakaamuru pesa hiyo iwekwe. Nao pia wanatudanganya? Kuwekeza kwenye taasisi kubwa kama Simba, sidhani kama usipoweka mzigo serikali itakaa kimya kwa sababu nayo inahitaji mapato yake mbalimbali kisheria kutokana na hizo bilioni 20.

Sasa nao wawe kimya ili kumsaidia Mo, kuwaongopea Wanasimba na Wananchi kwa ujumla?

Je, wanaohoji hilo kama hawamuamini Mo, pia hawaiamini serikali? Au wanaiamini na wanajua, ila wanafanya hivi kwa sababu tu ya kuwaaminisha mashabiki wa soka, ili kutengeneza mazingira ya Mo kutoaminika? Na je, kama ni hivyo ni kwa sababu ya kimaendeleo ya klabu na mpira au maslahi binafsi?



Makamu Mkuu wa Chuo cha Kilimo na Mifugo Kaole, kilichopo Bagamoyo mkoani Pwani Maximillian Sarakikya (wa tatu kulia) akifafanua jambo kwa baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya bia ya Serengeti waliotembelea chuo hicho mwishoni mwa wiki. Wengine katika picha ni wanafunzi wa chuo hicho ambao ni wanufaika na programu ya ufadhili wa masomo inayojulikana kama Kilimo Viwanda. **PICHA: MPICHA WETU**

# NBC yatoa gawio bil. 4.5/- serikalini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imetoa gawio la Sh. bilioni 4.5 kwa serikali ikiwa ni faida iliyopata kwa mwaka 2020/21.

Akipokea gawio hilo kwa niaba ya serikali, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliipongeza NBC kwa kuendelea kuimarika na kuongeza faida kila mwaka.

"Nimefarijika sana kusikia kuwa kwa mwaka 2021 Benki ya NBC ilipata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 60, ambalo ni ongezeko la asilimia 702 kutoka faida ya bilioni 6.2 iliyopatikana mwaka 2020. Haya ni mafanikio makubwa sana...hongereni sana," alisema Dk. Nchemba na kuongeza:

"Zaidi nawapongeza sana kwa mchango wenu katika uchumi wa Taifa. Hakika nyinyi ni mfano wa kuigwa. Uwekezaji wenu katika jamii umekuwa chachu kubwa ya maendeleo. Napongeza sana".

Waziri Nchemba alisema ni jambo la kujivunia kuona kuwa serikali ambayo ina umiliki wa asilimia 30 ya hisa za Benki ya NBC, inapata kiasi cha Sh. bilioni 4.5 kama gawio lake.

Alisema pesa hizo zitatumika kugharamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kuboresha huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na maji.

Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alisema kutolewa kwa gawio hilo kunathibitisha kuwa uamuzi uliofanywa na serikali katika kubinafsisha mashirika ya umma yalikuwa ni maamuzi yenye tija. "Niliwahi kufanya kazi NBC miaka kadhaa iliyopita. Hadi naondoka nakumbuka gawio lilikuwa ni Shilingi bilioni moja, lakini miaka kadhaa baadaye tunapokea zaidi ya mara nne ya gawio lile. Hii ni hatua kubwa na niwapongeze Benki ya NBC kwa hatua hii kubwa," alisema Mafuru. Alizitaka taasisi zinazomilikiwa na serikali kwa asilimia 100 kujifunza kutoka kwenye mashirika yanayomilikiwa kwa ubia na serikali ili kuona ni jinsi gani yatajiendesha kwa faida.

Alisema kuwa sekta ya benki nchini kwa sasa imekua kwa asilimia 10 na kufanya sekta hiyo kuwa taasisi muhimu inayogharamia shughuli za uchumi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, aliishukuru serikali kwa kuiwezesha benki hiyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na kueleza kuwa mwaka 2021 NBC imetoa kodi Sh. bilioni 20 serikalini pamoja na kutoa gawio hilo. Alisema NBC imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta mbalimbali ikiwamo uwekezaji wa zaidi ya Shilingi bilioni moja iliyotumika katika misaada ya kijamii na uwekezaji wa zaidi ya shilingi bilioni tisa zilizotolewa kwenye mchezo wa soka kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kaimu Msajili wa Hazina, Joseph Mwaisemba, alisema hadi Mei mwaka huu ofisi yake ilifanikiwa kukusanya maduhuli ya Sh. bilioni 691, inahitaji Sh. bilioni 86 ili iweze kufikia lengo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, aliipongeza NBC kwa kutoa gawio hilo pamoja usimamizi mzuri wa serikali uliosababisha kupatikana kwa gawio hilo.

Alisema gawio hilo litasaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi ya serikali iliyolenga kuwanufaisha wananchi katika nyanja mbalimbali.

# Zawadi 500,000/- ukifichua wezi miundombinu umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Nchini (TANESCO), limetangaza zawadi ya Sh. 500,000 kwa mwananchi atakayewafichua wezi wa miundombinu ya umeme.

Shirika hilo limesema Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga ni kinara kwa kuhujumu miundombinu ya umeme kwa kuiba mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma na kusababisha hasara ya Sh. milioni 400 katika kipindi cha miezi mitatu.

Lengo la kutoa fedha hiyo ni kuhakikisha miradi ya TANESCO inalindwa na kuwanufaisha wananchi na ikibainika katika maeneo yao kumehujumiwa miundombinu, serikali itaanza kuchukua hatua kwa kamanda wa jadi (Sungusungu).

Ofisa Usalama Kanda ya Magharibi wa TANESCO, Saidi Songwe, aliyabainisha hayo jana wakati wa kikao kazi cha kushirikisha jeshi la jadi (Sungusungu) kutoka kata 58 za wilayani humo katika kulinda miundombinu ya shirika lisihujumiwe.

Alisema Kanda ya Magharibi inaundwa na mikoa minne ya Shinyanga, Tabora, Katavi na Kigoma, lakini Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Kahama ndiyo unaongoza kwa kuhujumu miundombinu ya umeme na kusababisha wateja kuendelea kukosa huduma.

Alisema tatizo la hujuma ya miundombinu limesababisha pia baadhi ya viwanda kusimamisha uzalishaji na hivyo kulikosesha shirika mapato.

Songwe alisema yanapotolewa mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma wanaporejesha inawagharimu Sh. milioni 12 na wanapochelewa kurejesha kwa wakati kwa kutokujua inawagharimu Sh. milioni 400 na ndiyo sababu ya kuwashirikisha Sungusungu kwa ajili ya ulinzi kwenye maeneo yao.

"Serikali inatoa fedha nyingi katika kusogeza huduma ya nishati kwa wananchi, baadhi yao wanaihujumu kwa kuiba nyaya za kopa na mafuta kwenye transfoma ambazo zinasaidia kulinda uhai wa transfoma na kufanya kazi vyema," alisema Songwe.

Naye Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Shinyanga, Grace Ntungi, alisema matukio ya wizi wa vifaa katika transfoma yameshika kasi katika Kata ya Kagongwa na Bulyanhulu hali ambayo inasababisha umeme kukatika mara kwa mara. Alisema mpaka sasa zaidi ya transfoma 40 zimeshaharibiwa kwa kuibwa mafuta na nyaya za kopa na wizi wa mafuta na kuwaomba sungusungu katika maeneo yao kulinda na kukomesha vitendo hivyo visiendelee kujitokeza.

Ntungi alilitaka jeshi hilo kwa kushirikana na polisi kata waliopo, kuwa mstari wa mbele kutokomeza vitendo hivyo kwa sababu wanaofanya wizi wa namna hiyo ni watu wanaoishi nao ndani ya jamii na ikiwezekana kukomesha tabia hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwataka sungusungu kufanya mikutano katika maeneo yao na kuwaeleza wananchi umuhimu wa kulinda miundombinu ya umeme.

Kiswaga aliwataka sungusungu hao wanapoona mtu (fundi) anapanda kwenye nguzo za umeme wamhoji kujua uhalali wake na kutoa taarifa katika ofisi zao kujiridhisha ili kumaliza tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Sungusungu wilaya, Muzari Kashindya, alisema atahakikisha anafanya mikutano ya mara kwa mara ya kulikumbusha wajibu jeshi lake la jadi ikiwamo kulinda miundombinu.

# Wanafunzi 27 Chuo Kilimo kupata ufadhili

**Na Frank Monyo**

WANAFUNZI 27 kutoka katika Chuo cha Kilimo na Mifugo Kaole, Bagamoyo mkoani Pwani, wamekabidhiwa vyeti vya ufadhili wa masomo na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) ili kuwawezesha vijana kuwa na ushiriki mpana zaidi katika kilimo.

Akiongea jana wakati wa kukabidhi vyeti hivyo katika chuo cha Kilimo na Mifugo Kaole, chini ya programu ya Kilimo Viwanda, Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha alisema, SBL inatambua umuhimu wa vijana kushiriki katika kilimo.

"Vijana ambao tunawafadhili chini ya programu ya kilimo viwanda, watakwenda kuongeza nguvu kwenye sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Mchango wao utakuwa muhimu sana katika kuhakikisha kilimo chetu kinakuwa na tija," alisema Wanyancha.

Wanyancha alisema kuwa SBL hutumia malighafi zinazotokana na kilimo kutengenezea bia zake ikiwa ni pamoja na shayiri, mtama na mahindi na kuongeza kuwa uwapo wa wataalamu wa kutosha utasaidia upatikanaji wa malighafi hizo ambazo mahitaji yake yamekuwa yakiongezeka.

"Mahitaji yetu ya malighafi yanaongezeka kila mwaka. Mwaka 2021 kwa mfano tulinunua tani 18 za malighafi ambazo ni sawa na asilimia 80 ya mahitaji yetu kwa mwaka. Lengo letu ni kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025," alisema.

Kupitia programu ya kilimo viwanda, SBL imeshatoa ufadhili kwa wanafuzi zaidi ya 200 wanaosomea masomo ya kilimo katika vyuo vinne ambavyo ni Kaole cha Bagamoyo, Kilacha cha Moshi, Mt. Maria Goretti cha Iringa na Igabiro kilichopo Muleba mkoani Kagera.

Mkuu wa Chuo cha Kaole, Sinani Simba aliishukuru SBL kwa kutoa ufadhili kwa wanafunzi ambao amesema pasipo msaada huo wengi wao wangeshindwa kumaliza masomo yao kutokana na changamoto ya kushindwa kulipa ada.

"Mchango wa SBL siyo tu unawasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia duni kupata fursa ya kuendelea na masomo, bali pia unasaidia kukuza sekta ya kilimo hapa nchini kupitia kuongeza wataalamu ambao takwimu zinaonyesha ni wachache ukilinganisha na mahitaji," alisema.

# Mahakama ya Rufani yatupa ombi kampuni kumiliki kiwanja

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Rufani imetupilia mbali ombi la Kampuni ya J.W. Ladwa (1977) Ltd, iliyokuwa ikitaka kusimamisha utekelezaji wa amri ya Mahakama Kuu, iliyotangaza Kampuni ya Bansons Enterprises Ltd kuwa ni wamiliki halali wa kiwanja kilichopo Chang'ombe, jijini Dar es Salaam.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na jopo la majaji watatu, Jaji Ferdinand Wambali, Rehema Kerefu na Abrahaman Mwampashi.

Majaji hao walitoa uamuzi huo dhidi ya J.W. Ladwa (1977) Limited, mwombaji, baada ya kushindwa kukidhi masharti mawili yaliyotolewa chini ya kanuni za Mahakama ya Rufani ya kuonesha hasara ambayo wangepata.

"Tunaona mwombaji ameshindwa kukidhi masharti yote mawili yaliyoainishwa chini ya kanuni ya 11 (5) (a) na (b) ya kanuni za Mahakama ya Rufani na hivyo hajaonesha sababu za msingi za kukubaliwa kwa maombi hayo. Kwa hivyo, ombi hilo limetupwa."

Katika uamuzi wao, majaji walikubaliana na Wakili wa mlalamikiwa Thomas Brash, kwamba mwombaji hajaweza kuthibitisha vya kutosha hasara kubwa inaweza kumsababishia iwapo ombi hilo litakataliwa.

Kuhusu malipo ya Sh.milioni 10 majaji walibainisha kuwa mwombaji alijitolea kusalimisha vyeti viwili vya umiliki wa viwanja ambavyo ni namba 977228 kiwanja No. 240 Kitalu "K" namba 124738 kiwanja namba 223 kitalu "K" vyote vipo Mapinga Bagamoyo Mjini.

Kwa mujibu wa majaji hao, uhusiano kati ya mwombaji na mali mbili zilizotolewa kama dhamana ya malipo ya Sh. milioni 10, ilivyoamriwa na Mahakama Kuu haujaoneshwa na kuthibitishwa katika hati ya kiapo.

Aidha, walibaini kuwa hakukuwa na ushahidi wowote kwenye kumbukumbu ya maombi hayo kwamba mmiliki wa kiwanja hicho, yaani, Simba Motors (T) Limited, ameridhia mali zake kutolewa kama dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa amri ya Mahakama hiyo.

"Kwa hiyo ni maoni yetu kwamba kwa kuzingatia kanuni ya 11 (5)(b) ya kanuni za Mahakama ya Rufani pale dhamana itakayotolewa ni ya mali, mali iliyotolewa lazima iwe ya mwombaji au kama sivyo, basi lazima iwe na kibali kutoka kwa mmiliki ili mali itolewe hivyo.".

Katika hukumu yake, Mahakama Kuu ilimtangaza mlalamikiwa katika rufaa hiyo, Bansons Enterprises Limited, kuwa mmiliki halali wa kiwanja namba 273 kitalu "C" kilichopo eneo la Chang'ombe Dar es Salaam na kumtaka mlalamikiwa kuondoka eneo hilo na kulipa Sh. milioni 10 kama fidia kwa kosa la kuvamia eneo hilo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama akizungumza na Wananchi wa Kijiji cha Ilongero, mkoani Singida wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) ilipotembelea kijiji hicho kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF).

## Watumishi TRA kortini madai uhujumu uchumi

**Na Said Hamdani,** KILWA MASOKO

WATUMISHI wawili wa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) na mfanyabiashara, wilayani Kilwa, mkoani Lindi, wamefikishwa mahakamani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa makosa ya matumizi mabaya ya mamlaka na uhujumu uchumi.

Washtakiwa hao ni watumishi kitengo cha Forodha TRA wilayani humo, Sultani Nassoro (28) na Silvery Maximilian (53) pamoja na mfanyabiashara Kata ya Kivinje, Athumani Ahmadi Simba (37).

Akiwasomea mashtaka mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Innocent Sotter, Mwanasheria wa TAKUKURU Mkoa wa Lindi, Osborn Poris, alidai Februari 4, 2019, Bandari ya Kivinje, washtakiwa walijihusisha na vitendo kinyume na sheria.

Alidai, washtakiwa Nasoro na Maximilian, katika shtaka la kwanza wanadaiwa kutumia vibaya mamlaka waliyopewa.

Kosa la pili ni kufanya udanganyifu wa ukadiriaji kodi usio sahihi na kosa la tatu ni kuisababishia Mamlaka hasara.

Katika kosa la nne linalomhusu mfanyabiashara Simba, mwanasheria huyo alidai ni kukwepa kulipa kodi halali ya serikali.

Washitakiwa wote kwa pamoja wamekana makosa yao na wapo nje kwa dhamana. Kesi hiyo imepangwa kutajwa tena Juni 20, mwaka huu.

Imedaiwa kuwa Simba ni mfanyabiashara katika mji mkongwe wa Kivinje, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, anayedaiwa kuingiza mafuta ya kupikia madumu 500 ya lita 20 kila moja na yaliyokadiriwa na kulipiwa kodi ni 200 pekee.

# 'Walionufaika TASAF, wapisheni wenzenu'

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imewataka wanufaika wa ruzuku waliodumu muda mrefu, wajitoe katika mpango wa kunusuru kaya maskini ili kuwapisha wapya wenye mahitaji zaidi ya kuukabili umasikini, unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora, Jenister Mhagama, alisema hayo jana, alipokutana na walengwa wa TASAF, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, kwenye mkutano wa hadhara, uliofanyika makao makuu ya Tarafa ya Ilongero Kupitia mkutano huo ulioandaliwa kwa ajili ya Kamati ya Bunge, Utawala Bora na Serikali za Mitaa, Waziri Mhagama, alisema sasa ni wakati mwafaka kwa wanufaika wa TASAF waliodumu muda mrefu, kuwapisha walengwa wapya ili nao wanufaike na mpango huo.

"Tumshukuru sana Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan, kutufutia fedha kwa ajili ya kaya maskini, ninyi watu wa Ilongero mkiwa mojawapo ya wanufaika... sasa niwaombe, wale walioanza muda mrefu kwenye mpango huu, watoke ili waingie wengine wenye mahitaji zaidi," alisema Mhagama.

Awali, akiongea katika mkutano huo, Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Eliya Dighah, alisema mpango umetekelezwa vyema Singida Vijijini, yakiwamo malambo mawili yaliyokamilika kupitia fedha za TASAF.

Alisema, baada ya vijiji 40 vilivyopo kwenye mpango huo kunufaika na mpango huo kwa kipindi kirefu, sasa ni muda mwafaka kwa vijiji vingine 48 vilivyopo katika halmashauri hiyo, kunufaika, baada ya serikali kuviingiza, na kuwa jumla ya vijiji 84.

Baadhi ya walengwa akiwamo Pili Mohamed, anayejihusisha na biashara ya uuzaji kinywaji cha kahawa na Tatu Rajabu, anayeuza mboga katika soko la Ilongero, walisema tangu waingie TASAF, wamefanikiwa ikiwamo kujenga nyumba na kujihusisha na ufugaji wa mbuzi.

Kutokana na mafanikio hayo, walengwa hao walitoa wito kwa wanufaika wengine nchini kujitahidi kubuni miradi mbalimbali itakayowainua kiuchumi kupitia fedha za ruzuku, ili ukifika wakati wa kutolewa kwenye mpango, waweze kumudu maisha yao.

# Wenye ulemavu wasio kipato kupewa kipaumbele matibabu

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

WATAALAMU wa afya katika Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera wametakiwa kuwahudumia kwa kutumia busara, watu wenye ulemavu wanaofika katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwapunguzia adha za kukosa matibabu kutokana na kutokuwa na kipato.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mradi wa utetezi na ushawishi kwa watu wenye ulemavu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kiafya uliofadhiliwa na Shirika la The Foundation For Civil Society kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 38.4, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk. Leontine Rwamulaza, alisema busara hiyo ya kuhudumiwa bila malipo iwalenge zaidi watu wenye ulemavu ambao watathibitika kutokuwa na kipato kabisa.

"Wakati tunasubiri mwongozo wa serikali wa utoaji huduma bure kwa kundi hili, wale watu ambao wana ulemavu ambao wamebainishwa kwa kitambulisho au maelekezo kutoka katika serikali ya kijiji wanapoishi huwa hawana uwezo wahudumiwe, lakini hata ambao hawana utambulisho wowote mkajiridhisha kuwa wana uhitaji huo, wasiachwe," alisisitiza Dk. Rwamulaza.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo (CHAWATA), mkoani Kagera, Laurian Pankras, aliiomba serikali kutoa elimu ya ujasiriamali kwa watu wenye ulemavu ili waweze kunufaika na mikopo itokanayo na asilimia mbili za mapato ya ndani ya halmashauri, na kuwapunguzia utegemezi.

"Nyinyi watu wa kutusemea mnasema walemavu pambaneni kwa hiyo twende tuandamane, leo hii pesa ambazo tumezipata kuelimisha watu ambao wanatunyanyapaa zingekuwa zinatumia kuelimisha watu wenye ulemavu kuhusu ujasiriamali, kwa sababu wanakosa kukopa maana hawana elimu hiyo," alisema Pankras.

Wakili wa kujitegemea, Dunstan Mutagahywa, anayetoa elimu ya kisheria kwa kundi hilo, alisema kuwa ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapatiwa tiba bure, halmashauri zinaweza kutunga sheria ndogo ambazo zitaweka utaratibu namna gani watu hao wanaweza kutibiwa bila malipo.

"Kuna uwezekano kama halmashauri ya Wilaya ya Muleba ikiona kwamba imefika wakati wanaweza kutunga sheria ndogo za kuwahudumia watu wenye ulemavu bure ni sahihi, maana wakifanya hivyo wataingia katika bajeti yao na kumwezesha mganga mkuu kutelekeza hilo, na inawezekana," alisema Wakili Mutagahywa.

Kwa mujibu wa Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye ulemavu (Shivyawata), mkoani humo, Sweetbert Mushanga, utafiti uliofanywa na shirikisho hilo ulibaini kuwa Wilaya ya Muleba inaongoza kwa kutoa huduma duni kwa kundi hilo.




Mkurugenzi wa Biashara Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa akikabidhiana mkataba na Mwenyekiti wa migahawa ya Samaki Samaki, Carlos Mella (Kalito) wakati wa hafla ya kusaini mkataba kati ya Vodacom na migahawa hiyo itakayotoa zawadi kwa wateja wa Vodacom watakaolipia kwa kutumia M-Pesa watarudishiwa asilimia 10 ya malipo yao na pia wateja wote watapata huduma ya bure ya WiFi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtwara yaanza udhibiti wizi dawa za serikali

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

VITUO vya huduma ya afya binafsi na serikali mkoani Mtwara vimeagizwa kusitisha matumizi ya fomu namba mbili C ambayo ni maalumu kwa ajili ya uchukuaji dawa kwenye maduka ya nje ya dawa ili kukomesha wizi na uimarishwaji wa uwapo dawa kwenye vituo hivyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana wilayani hapa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Dk. Hamadi Nyembea kwa kushirikiana na Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani humo, Dk. Adolf Kahamba kwenye kikao kazi cha kupeana taarifa ya namna bora ya uendeshaji vituo vya afya binafsi na jinsi ya kusajili vituo hivyo.

Agizo hilo ni utekelezaji wa serikali kupitia Wizara ya Afya ifikapo Juni Mosi, mwaka huu fomu hiyo isitumike tena.

Dk. Kahamba alisema serikali imetoa maelekezo kuanzia sasa matumizi ya fomu namba mbili C iliyokuwa ikitumika katika vituo vya afya binafsi na serikali kwa ajili ya kuchukua dawa kwenye maduka ya dawa kwa ajili ya wagonjwa wanaotumia bima ya afya kutotumika. Alisema tayari serikali imeshatoa wajibu kwa waganga wakuu wa mikoa kufuatilia na kutekeleza agizo hilo la usitishwaji wa fomu hizo.

Uamuzi huo umekuja baada ya kuona matumizi yake yanakiuka taratibu za serikali na kusababisha ubadhirifu wa dawa za serikali kupitia fomu hizo na ujazaji wake kuomba dawa ulikuwa sio wa halisia. Vile vile, alisema kwa upande wa vituo vya afya vya serikali pia hadi kufika Julai Mosi hazipaswi kutumia fomu hizo kwa wateja walioko katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Meneja NHIF, Kahamba alisema kuwa mfuko huo unaendelea kusisitiza agizo la serikali la kusitisha matumizi ya fomu hizo katika vituo vya afya ambavyo ni wateja wanachama wa bima ya afya hadi serikali itakapotoa maelekezo mapya.

Alisema vituo vyote vya afya Mkoa wa Mtwara ambavyo vinafomu hizo vinapaswa kuzirejesha ofisi za NHIF na usitishwaji huo utasaidia kukomesha wizi wa dawa za serikali na uimarishaji wa upatikanaji dawa kwenye vituo hivyo.

Naye Dickson Takatuka mtoa huduma za afya katika zahanati binafsi ya Chikumba, alipongeza serikali kwa hatua hiyo ya kusitisha fomu hiyo ili sasa kuanza kuwa na nguvu kubwa ya kuwa na dawa nyingi kwa ajili ya wateja wao.

# CDTI-Ruaha wajitosa ujenzi zahanati ya kijiji

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WANANCHI wa Kijiji cha Ikuvilo katika Kata ya Luhota wilayani Iringa, wamepongeza Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Ruaha (CDTI- Ruaha) na wanafunzi kwa kuungana na serikali ya kijiji hicho kuhamasisha ujenzi wa zahanati ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Walisema ujio wa zahanati hiyo utapunguza adha ya wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za kimatibabu na wajawazito kujifungulia nyumbani na vifo vya watoto vitokanavyo na uzazi.

Wananchi hao walisema kijiji chao pamoja na vijiji vinavyozunguka kijiji chao kwa muda mrefu vinakabiliana na tatizo la ukosefu huduma za afya na kulazimika kutembea mwendo mrefu zaidi ya kilometa 18 kutafuta matibabu katika maeneo mbalimbali.

Kijiji cha Ikuvilo kinazungukwa na Kijiji cha Tagamenda upande wa kaskazini, Nyabula upande wa Mashariki na upande wa kusini Kijiji cha Idunda, vyote havina zahanati.

Jane Njavike alisema wajawazito wengi wanapata shida wakati wa kujifungua kwa kujifungulia njiani kutokana na kutembea umbali mrefu zaidi ya kilometa 18.

Alitoa mfano wa binti yake aliposhikwa na uchungu wa kujifungua alikodi bodaboda, lakini alijifungua mtoto kabla ya kufika hospitali ya Ipamba ambayo ni teule ya Wilaya ya Iringa.

"Kwa kweli tunakipongeza Chuo cha Mandeleo ya Jamii CDTI Ruaha kwa kuungana na serikali ya Kijiji cha Ikuvilo kwa kusikia kilio hicho cha zahanati....," alisema Njavike.

Alisema wanakodi gari toka Ipamba hadi Ikuvilo kwa gharama ya Sh. 30,000 ikingazitiwa hali duni ya kipato kwa wananchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikuvilo Meshack Mlawa, alisema wanaushukuru uongozi wa chuo cha maendeleo ya jamii Ruaha kwa kukubali kushirikiana katika ujenzi wa zahanati hiyo ambayo itasaidia kuboresha huduma za afya.

Alikiri kuwapo kwa vifo vya mama na mtoto kipindi unapofika muda wa kwenda kujifungua kutokana na kuifuata huduma ya afya mbali na tatizo la miundombinu.

Mlawa alisema kuwa Serikali ya Kijiji imefanikiwa kufyatua matofali 150,000 yatakayotumika katika ujenzi wa zahanati hiyo na kutimiza ndoto ya kijiji kuwa na huduma ya afya.

Alisema kijiji hicho kina wananchi 2,696 na kinapakana na vijiji vya Tagamenda, Nyabula na Idunda ambavyo pia havina zahanati.

CDTI kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji cha Ikuvilo Kata ya Luhota wameamua kujenga zahanati kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma ya afya kupatikana jirani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Chuo cha CDTI, Godfrey Mafungu, alisema wameamua kuunga mkono juhudi za serikali ya kijiji cha Ikuvilo na kushirikiana nao kuhakikisha wanapata huduma za afya.

Alisema kuwa malengo ya sasa ni kuhakikisha wanafanikisha ujenzi wa zahanati hiyo baada ya miezi sita huku akitoa rai kwa wananchi kuchangia shughuli za maendeleo ya kijiji.

Mafungu alisema kuwa maendeleo ya kijiji cha Ikuvilo yataletwa na wananchi wa kijiji hicho na wananchi wanatakiwa kujitoa kuhakikisha wanachangia maendeleo.

Alisema kuwa kukamilika kwa ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Ikuvilo kutachangia kuboresha huduma za afya na kupunguza vifo vya wananchi.

Rais wa Serikali ya wanafunzi wa CDTI Ruaha, Jacob Arusha, alisema kuwa lengo la kushirikiana na Serikali ya Kijiji cha Ikuvilo ilikuwa ni kusaidia kuboresha huduma ya afya kwa wananchi wa kijiji hicho.

Arusha alisema kuwa wameamua kufanya hivyo kwa kuwa wakiwa chuoni wanasomea masomo ambayo watajihusisha na maendeleo ya wananchi.

# Usajili vyeti vya kuzaliwa watakiwa kuzingatia sifa

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, amewaagiza viongozi wanaoshiriki katika usajili wa watoto kwa ajili ya kupatiwa vyeti vya kuzaliwa, wakiwamo Watendaji Kata na Wasajili kutoka katika vituo vya afya, kuhakikisha wanaopatiwa huduma hiyo ni wenye sifa.

Alitoa kauli hiyo mkoani hapa wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ya mpango wa usajili na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano mkoani humo unaoendeshwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa linalohudumia watoto (UNICEF) Tanzania, Serikali ya Canada, Kampuni ya simu za mkononi ya Tigo, Ofisi za Makatibu Tawala wa mikoa, Wakuu wa wilaya, Halmashauri na Manispaa.

Aliwataka watendaji hao kufanya kazi hiyo kwa weledi, uadilifu na uzalendo wa hali ya juu ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa uendeshaji wa kazi hiyo ya usajili na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano na kwamba serikali haitamfumbia macho yeyote atakayebainika kukwamisha mpango huo.

Alisema wakati wa utekelezaji wa mpango huo katika baadhi ya mikoa, imebainika kwamba baadhi ya wazazi hawana vitambulisho vya taifa na hivyo kutokuwa na uhakika kwamba watoto wanaowapeleka kusajiliwa ni wale wenye sifa stahiki.

"Wakati wa utekelezaji wa mpango huu katika mikoa ya Katavi na Rukwa, wazazi walitakiwa kuwasilisha kitambulisho cha taifa cha mzazi mmojawapo kwa ajili ya utambuzi, baadhi ya wazazi walibainika kutokuwa navyo na hivyo kutokuwa na uhakika juu ya uraia wao na hadhi yao na hivyo kusababisha watoto wao kukosa haki ya kutambuliwa," alisema Makondo.

"Ili kuhakikisha watoto wanaosajiliwa ni wenye sifa stahiki, serikali pamoja na mambo mengine, iliamua pamoja na mamlaka za usajili wa vizazi kutekeleza majukumu yake, ni vyema vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na mamlaka nyingine za utambuzi zishirikiane kikamilifu katika kazi hiyo."

Alisema pamoja na mambo mengine, pia serikali iliamua wazazi wa watoto wanaotoka katika maeneo yenye kambi za wakimbizi, taarifa zao zithibitishwe kupitia kwa maofisa makazi katika kambi hizo.

"Kwa namna ya pekee, serikali inaipongeza RITA, ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya pamoja na mamlaka za serikali mitaa katika mikoa yote ambayo mpango unatekelezwa. Serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na wadau wa maendeleo ikiwamo UNICEF, Serikali ya Canada na Kampuni ya simu za mkononi ya Tigo katika mpango huu," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Angela Anatory, alisema chimbuko la kuanzishwa kwa mpango huo ni uwapo wa kiwango kidogo cha wananchi waliosajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa nchini.

Alisema lengo la mpango huo ni kutatua changamoto zilizokuwapo katika mfumo wa awali, kuboreshwa zaidi na kusogeza karibu na maeneo ya makazi ya wananchi pamoja na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya mama na mtoto na ofisi za watendaji Kata.

Pia, ni kuondoa ada ya cheti kwa watoto hao wanaosajiliwa kupitia mpango huo na kuimarisha mfumo wa kutuma na kuhifadhi taarifa za waliosajiliwa kwa kutumia TEHAMA.

"Kwa ujumla mafanikio ya utekelezaji wa mpango huu katika mikoa iliyotangulia ni makubwa na 7,549,878 wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Alisema tangu kuzinduliwa kwa mpango huo Juni mwaka 2015, idadi ya usajili wa watoto chini ya miaka mitano imepanda kutoka asilimia 13 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 62 mwaka 2021 na mikoa ambayo imekwishanufaika na mpango huo mpaka sasa ni 22.




Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare, (Kulia) akibadilishana nyaraka za mkataba wa makubaliano na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Mibako Mabubu, ambapo mgodi huo umetenga Shilingi Bilioni 1.9 kwa ajili ya utekelezaji miradi ya kijamii kwenye halmashauri hiyo katika kipindi cha mwaka huu .Hafla ya kusaini makubaliano hayo ilifanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani aomba msaada wa kukamilisha nyumba ya yatima

**Na Julieth Mkireri,**

DIWANI Viti Maalumu (CCM), Lydia Mgaya ameomba wadau kujitokeza kusaidia umaliziaji wa nyumba aliyojenga kwa ajili ya watoto yatima wanaoishi katika Mtaa wa Bamba, Kata ya Kongowe, Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mjini hapo, Lydia alisema aliamua kuanza kujenga nyumba hiyo baada ya kutembelea familia ya watoto watano ambao wazazi wao walifariki na kuwaacha wakiwa wadogo.

Diwani huyo alisema kwa sasa amekwama katika hatua ya umaliziaji na zinahitajika Shilingi milioni saba kununua vifaa na kuomba msaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

"Nilikutanishwa na familia hii na wanawake wa Kongowe ambao waliona nikiwa na wazee tukikandika nyumba zao za udongo ambazo zilikuwa zimechoka na kuhitaji kukarabatiwa wakanieleza kuhusiana na watoto hawa yatima," alisema.

Alisema kupitia wadau mbalimbali waliomuunga mkono amefanikisha kushirikiana nao kujenga nyumba hiyo ambayo kwasasa inahitaji vifaa kwa ajili ya umaliziaji.

Mmoja wa watoto hao, Mohamed Hamis, alisema baada ya wazazi wao kufariki walibaki na bibi yao ambaye naye hakuwa na uwezo wa kuwahudumia huku wakiwa wanaishi katika nyumba mbovu ambayo ilikuwa inavuja na ilikuwa hatarini kubomoka kutokana na uchakavu.

"Tuliachwa na wazazi wetu mimi nikiwa darasa la tano nililazimika kufanya kibarua kwa mtu kwa kuuza kuku ili wadogo zangu, dada yangu na bibi waweze kula, niliendelea kufanya hivyo mpaka nilipomaliza kidato cha nne ambapo nilifeli mitihani yangu kwa kukosa muda wa kujisomea," alisema Mohamed.

Alisema kwa sasa anajishughulisha na vibarua vya kulima na kusaidia mafundi ujenzi ili ndugu zake wapate chakula huku wakiishi kwenye nyumba ya kupanga wakisubiri wanayojengewa na diwani huyo ikamilike.

Bibi wa watoto hao, Mwansiti Said, alimshukuru Diwani Lydia kwa hatua ya kuithamini familia hiyo na kuwajengea nyumba ya kudumu ambayo ikikamilika itaisitiri familia hiyo.

Aliomba wadau kushirikiana na diwani huyo kwa michango ya fedha na vifaa ili wakamilishe ujenzi wa nyumba hiyo kwa kuwa hata sasa nyumba wanayoishi haipo katika hali nzuri.

Binti wa familia hiyo anadaiwa kukatisha masomo kutokana na hali duni ya maisha iliyosababisha kujiingiza kwenye vishawishi na baadaye kupata mimba.

# 'Wajengeeni watoto utamaduni kuhifadhi mazingira'

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa Kibaha wamehamasishwa kujijengea utamaduni wa kupanda miti ili kuweka mazingira katika hali ya kuvutia na kuyatunza.

Mkuu wa Idara ya Usafi wa Mazingira Manispaa ya Kibaha, Ally Khatibu, alitoa hamasa hiyo juzi wakati wa upandaji miti katika Zahanati ya Bokotimiza Kibaha, iliyowashirikisha watoto kutoka shule mbalimbali katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Aliwasihi viongozi kushirikiana na wazazi kuwafundisha watoto wao utamaduni wa kuhifadhi mazingira ili kukuza kizazi kinachofuata misingi ya kupanda miti.

Alisema ni wajibu wa kila mwanajamii kuguswa kutambua kuwa mazingira ni mambo yote yanayo athiri ukuaji au uwapo wa viumbe hai, akitolea mfano hewa, maji na ardhi inapaswa kuchukua hatua ya kuwafundisha watoto kupanda miti.

"Kwa wiki nzima tulikuwa na kampeni ya mazingira duniani na wenzetu wa Bokotimiza walishirikiana na Shule ya Bright Lise School na kama mnavyowaona hawa watoto wanafundishwa na watakuwa wakitambua hivyo nawaomba viongozi na wazazi kuwafundisha watoto wetu," alisema.

Mkurugenzi wa Shule ya Lise, Yusuph Chanika, alisema kampeni ya kupanda miti ni endelevu na kwenye shule hiyo watoto wanafundishwa misingi ya kupenda mazingira yao kwa kupanda miti.

"Kwa leo tumechimba mashimo 120 na kupanda miti na kampeni ya upandaji itakuwa endelevu ili kutunza mazingira ya mji wetu wa Kibaha na natoa wito kwa wananchi wote kuhakikisha kwenye eneo analoishi anapanda miti," alisema Chanika.

Mkuu wa shule hiyo, Mainda Chanyika, alisema wameamua kuwashirikisha watoto hao katika utunzaji mazingira ili utamaduni huo uwe ndani ya mioyo yao kwa sababu uharibifu wa mazingira ni mkubwa. "Kila mtoto atakuwa na mti wake kila siku atakuwa anakuja na chupa ya lita moja kumwagilia mti wake mwisho wa siku utakuwa na kupata kivuli," alisema.

Mwakilishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano ambaye pia ni Balozi wa Kampeni ya upandaji miti Kitaifa, Richard Kalongola, alisema jukumu lao kubwa ni kuwahamasisha wananchi kupendezesha mazingira ili kutimiza azma ya serikali. "Na tumekuwa tukitoa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira pamoja na uoteshaji wa miti leo tupo Kibaha, lakini tumekuwa tukizunguka nchi nzima na hapa tuliwapa elimu," alisema.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yalifanyika jana yakiongozwa na kaulimbiu 'Dunia ni Moja' kitaifa yalifanyika Dodoma.

# Nipashe Spotika




SAJILI KUBWA 5 ZILIZOTHIBITISHWA TAYARI KUELEKEA MSIMU UJAO UK. 12-13




BENZEMA

# WACHEZAJI WA5 WALIOKOSA PENALTI NYINGI 2021-2022

**LONDON,** England

MSIMU wa 2021-22 haujawa mfupi kutokana na matukio ya aina yake kwenye michezo kadhaa. Penalti mara kwa mara imekuwa muhimu katika michezo mikubwa. Wakati baadhi ya wachezaji wakizifunga kwa kujiamini sana, wengine wamekosa kile kinachohitajika kutoka mahali hapo.

Wakati huo huo, wachezaji wengine wamefunga nyingi, lakini pia wamekosa chache. Bila kujali, inahitaji mishipa isiyoweza kutetereka kuweka mpira nyavuni, haswa katika wakati mgumu ambao unaweza kuupa uhai mchezo au kuvunja. Kuna nyota wachache ambao wameshindwa kufanya hivyo msimu huu. Kwa maelezo hayo, tuwatazame wachezaji watano waliokosa penalti nyingi zaidi Ulaya msimu huu wa 2021-22.

Kumbuka: Ni Ligi tano Bora za Ulaya pekee ndizo zimezingatiwa hapa, twende sasa...

**#5. Pierre-Emerick Aubameyang - 2**

Pierre-Emerick Aubameyang alipata mapinduzi makubwa katika kipindi cha pili cha msimu baada ya kukamilisha uhamisho wa kwenda Barcelona kutoka Arsenal Januari.

Nyota huyo wa Gabon alikuwa na mzozo na kocha wake, Mikel Arteta katika klabu ya Arsenal kutokana na matatizo yake ya kinidhamu katika klabu hiyo. Hata hivyo, nyota huyo wa Afrika alifufua namba zake pale Nou Camp, kwa kufunga mabao 11 na kutoa pasi moja ya bao katika michezo 16 ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Ingawa pia alikuwa mfungaji bora zaidi pale kwenye dimba la Emirates kabla ya kuondoka kwenda Hispania, lakini pia alikuwa na rekodi mbaya ya penalti msimu huu.

Katika kipindi cha kwanza cha msimu wa sasa, Aubameyang alikosa mkwaju wa penalti dhidi ya Aston Villa kabla pia kushindwa kufunga kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Watford. Lakini kutokana na kwamba amepata viatu vyake vya kufunga tena, labda ulikuwa uamuzi mzuri kuihama klabu hiyo katika dirisha la dogo la usajili la majira ya baridi.

**#4. Bruno Fernandes- 2**

Bruno Fernandes amefanya kazi kwa bidii sana pale Manchester United msimu huu, lakini pia alikuwa na wakati mgumu kwa 'Mashetani Wekundu' hao. Ingawa kuna sababu nyingi nyuma ya kiwango chake duni, ukosefu wa kujiamini hakika ndio sababu kubwa.

Nyota huyo wa Ureno alikuwa akiivutia timu yake mwanzoni mwa msimu, lakini aliwapa mashabiki mshituko mkubwa dhidi ya Aston Villa, Septemba mwaka jana. Baada ya bao la dakika za lala salama la Villa, Fernandes alipata nafasi ya kusawazisha katika muda wa ziada, lakini akapiga shuti la penalti juu, na kuwaacha Man United wakiondoka na kichapo chao cha kwanza kwenye ligi msimu huu.

Mchezaji huyo pia alikosa mkwaju wa penalti muhimu alipopata nafasi ya kusawazisha dhidi ya Arsenal. Bao lake lingeweza kuitia moyo timu yake kusonga mbele na kutafuta mshindi, lakini badala yake aliwashusha moyo na kwenda kufungwa mabao 3-1.

Kocha Erik ten Hag bila shaka atatafuta mtengenezaji mkuu wa mabao kwa klabu hiyo na kumbadilisha mpiga penalti baada ya Mholanzi huyo kuchukua mikoba hapo Old Trafford.

**#3. Lautaro Martinez- 3**

Licha ya kuwapoteza Romelu Lukaku, Achraf Hakimi na Antonio Conte msimu uliopita wa majira ya joto, Inter Milan wameweza kuleta changamoto ya ubingwa msimu huu. Wakati kocha anastahili sifa nyingi kwa hilo, Lautaro Martinez amekuwa muhimu sana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, amefunga mabao 21 na kutoa asisti tatu katika mechi 34 za Ligi Kuu Italia, Serie A, ambazo zimekuwa muhimu kwa mafanikio ya Nerazzurri hao msimu huu. Hata hivyo, kumekuwa na majuto pia, huku Martinez akishindwa kufunga penalti tatu msimu huu.

Ingawa makosa yake dhidi ya Udinese na Cagliari hayakuigharimu pointi timu yake, nyota huyo wa Amerika Kusini atasikitishwa na kukosa kwake dhidi ya AC Milan. Bao lake lingeweza kubadilisha sura ya mbio za ubingwa, lakini Inter Milan sasa watakuwa na matumaini kwamba, Martinez anaweza kuwa msaada tena mkubwa msimu ujao.

**#2. Karim Benzema- 4**

Karim Benzema amekuwa mfungaji bora zaidi barani Ulaya msimu huu. Mshambuliaji huyo wa Real Madrid amefikisha mabao 44 katika mechi 44 kwenye mashindano yote ikijumuishwa mabao 27 katika mechi 31 za Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Pia ametoa pasi za mabao 12.

Kwa hiyo, haishangazi kwamba 'Los Blancos' wamefuzu kwa ushindi wa ligi msimu huu na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kati ya mabao yake 27 ya ligi, saba amefunga kwa mkwaju wa penalti. Ingawa Mfaransa huyo amekuwa mtu makini sana langoni, lakini amekuwa mzembe wakati mwingine. Ili kuweka mambo sawa, Benzema amekosa penalti nne msimu huu, ambazo ni nyingi zaidi kwa msimu huu.

Angeweza kuwa na zaidi ya mabao 30 ya ligi kama angefunga penalti hizo, lakini mshambuliaji huyo wa kati hana uwezekano wa kuwa na majuto mengi kwa msimu huu.

**#1. Insigne ya Lorenzo- 4**

Lorenzo Insigne amekuwa mtumishi mwaminifu wa Napoli kwa muongo mmoja uliopita, lakini Muitaliano huyo anaihama klabu hiyo na kujiunga na FC Toronto majira ya joto. Lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, amefanya vema msimu huu, akiwa amefunga mabao 11 na asisti tisa katika mechi 31 za Serie A.

Hii imeihakikishia Napoli kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao wakiwa wamemaliza nafasi ya tatu na Insigne atajivunia ushindi huo. Lakini winga huyo amekuwa na uzoefu mkubwa wa mikwaju ya penalti msimu huu. Ingawa amefunga penalti tisa, pia amekosa nne.

## ISIKUPITE

KATIKA Ligi tano bora Ulaya, Manchester City ndiyo klabu iliyofunga mabao mengi zaidi msimu huu wa 2021/22 (mabao 150) kwenye mashindano yote ikifuatiwa na Liverpool (147), Bayern Munich (143) na Chelsea (122).



## Extra Time

# SAJILI KUBWA 5 ZILIZOTHIBITISHWA TAYARI KUELEKEA MSIMU UJAO



HAALAND

**LONDON,** England

FAINALI ya Ligi ya Europa Conference na Ligi ya Mabingwa Ulaya, msimu wa 2021-22, imekamilisha msimu.

**Baada ya msimu mgumu kama huo, ni wakati wa wachezaji na wafanyakazi kupumzika na kuchaji betri zao. Ingawa wiki zijazo zitakuwa zisizo na matukio mengi katika suala la hatua ya uwanjani, kutakuwa na ongezeko kubwa la shughuli nje ya uwanja.**

Wakati dirisha la usajili la majira ya joto likikaribia kufunguliwa, ni wakati wa maofisa wakuu wa klabu kujishughulisha na biashara na kufunga mikataba ya kufurahisha.

Leo, tutaangalia klabu tano ambazo zimetangulia kwenye foleni na tayari zimefanya usajili mkubwa. Wakati baadhi ya uhamisho huu umetangazwa rasmi, wengine wanatarajiwa kuthibitishwa katika siku chache zijazo.

### #5. Fabio Carvalho (Fulham kwenda Liverpool)

Liverpool walikaribia kumsajili mmoja wa nyota waliosisimua nchini England, Fabio Carvalho, kutoka Fulham katika dirisha la uhamisho la Januari. Usajili huo ulishindikana siku ya mwisho, lakini 'Wekundu' hao hawakumkosa kwa mara ya pili.

Jumatatu ya Mei 23, Liverpool ilitangaza kumsajili kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye atajiunga rasmi na klabu hiyo Julai Mosi, mwaka huu. Mkataba wa kinda huyo unamalizika mwishoni mwa huu.

Carvalho, ambaye alitia saini mkataba wa miaka mitano na Liverpool, alishiriki katika mechi 36 za ubingwa msimu wa 2021-22, akirekodi mabao 10 na asisti nane.

Katika timu iliyojaa wachezaji wakubwa wenye uwezo, itafurahisha kuona ni wapi Jurgen Klopp ataweza kumpa nafasi ya kutosha Carvalho.

### #4. Karim Adeyemi (Red Bull Salzburg kwenda Borussia Dortmund)

Timu ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Borussia Dortmund ina sifa ya kuibua na kulea washambuliaji wanaoweza kung'ara duniani.

Wamefanya hivyo hapo awali kwa Robert Lewandowski na Erling Haaland na wanaonekana kutaka kufanya vivyo hivyo kwa Karim Adeyemi. Baada ya kufurahishwa na kazi yake katika klabu ya FC Salzburg, Dortmund wamemsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kwa mkataba wa miaka mitano.

Dortmund wamelipa euro milioni 30 kwa ajili ya mchezaji huyo kwa klabu hiyo ya Austria.

Mshambuliaji huyo wa Ujerumani alikuwa na kiwango bora kwenye Bundesliga ya Austria wakati wa msimu wa 2021-22. Alitumia vema kasi yake, na uwezo wake, akafunga mabao 18 ya ligi na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 28.

Adeyemi, ambaye inadaiwa alivutiwa na "soka la kasi la Weusi na Manjano" hao utotoni mwake, ana kila kitu cha kuwa mfungaji bora.

Chini ya macho makali ya kocha mpya, Edin Terzic, Adeyemi anaweza kung'arisha mchezo wake zaidi na kuibuka kama mshindani thabiti wa kuichezea Ujerumani kwenye Kombe lijalo la Dunia nchini Qatar.

### #3. Franck Kessie (AC Milan kwenda Barcelona)

Vigogo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona wamepoteza mchezo wao wa kawaida siku za hivi karibuni, uwanjani na sokoni. Lakini hiyo haimaanishi kuwa hawawezi kuwashawishi wachezaji bora kujiunga na klabu yao kubwa.

Mshindi wa Kombe la Ligi Kuu Italia, Serie A, Franck Kessie ni mmoja wa wachezaji ambao wameamua kujiunga na washindi hao mara 26 wa LaLiga.

Kwa mujibu wa mwandishi maarufu wa habari za michezo, Fabrizio Romano, Barcelona ilimpatia mkataba mwishoni mwa Machi, na kumsajili kiungo huyo kama mchezaji huru. Romano aliongeza kuwa pande hizo mbili zimekubaliana juu ya mkataba wa miaka minne, ambao utamfanya mchezaji huyo kulipwa euro milioni 6.5 pamoja na nyongeza ya mshahara wa jumla.

Tangu ajiunge na AC Milan akitokea Atalanta mwaka 2019, Kessie amekuwa akionekana kwenye timu hiyo. Si tu kwamba yeye ni mchezaji bora wa mpira na mkabaji, lakini pia ana ustadi wa kufunga mabao.

Kwenye mechi 31 za Serie A katika msimu uliomalizika hivi karibuni, Kessie alifunga mabao sita.

### #2. Antonio Rudiger (Chelsea kwenda Real Madrid)

Mkubwa, mkatili, na mwepesi wa kuzuia, Antonio Rudiger bila shaka ndiye ufafanuzi kamili wa beki bora wa kati wa soka la kisasa.

Tangu ajiunge na Chelsea akitokea AS Roma mwaka 2017, Rudiger amekuwa akifanya vema katika kila mfumo ambao amekuwa akitumika. Hata hivyo, kipindi chake bora zaidi kilikuwa chini ya Thomas Tuchel, ambaye amemchezesha vema upande wa kushoto wa safu yake ya ulinzi ya wachezaji watatu.

Kwa ujumla, ameshiriki katika michezo 203 kwa 'The Blues' hao, akiandikisha mabao 12 na asisti saba.

Baada ya kuwatumikia Chelsea wanaotoka London Magharibi kwa bidii zaidi ya miaka mitano iliyopita, Rudiger anatarajiwa kuwa na mabadiliko ya mandhari msimu huu wa majira ya joto. Mjerumani huyo mkataba wake Chelsea unamalizika Juni 30, kumaanisha kuwa atakuwa huru kujiunga na klabu yoyote msimu wa majira ya joto.

Kwa mujibu wa Fabrizio Romano, Real Madrid ndio watakaomkumbatia beki huyo wa kati kwa mikono miwili msimu huu wa majira ya joto.

'Los Blancos' wameripotiwa kumsaijili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kwa mkataba wa miaka minne, bila masharti ya kuongeza msimu.

### #1. Erling Haaland (Borussia Dortmund kwenda Manchester City)

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England watatisha zaidi msimu ujao. Kama ilivyotangazwa na Manchester City wenyewe, wamefikia makubaliano ya kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Wamelipa kiasi cha pauni milioni 51 kuweza kuinasa saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway.

Uhamisho huo ulikamilika baada ya Man City kukubaliana na mchezaji huyo na atajiunga nao Julai Mosi mwaka huu.

City ina kikosi cha wabunifu zaidi duniani. Wakiwa na Haaland katika safu yao ya ushambuliaji, City wanapaswa kuboresha matokeo yao mbele ya lango.


Akiwa kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, amefunga mabao 62 katika mechi 67. Itafurahisha kuona jinsi atakavyofanya katika ligi ngumu duniani msimu ujao.

## Nukuu

"Kisingizio kibaya zaidi nilichowahi kusikia kutoka kwa mchezaji kuachana na klabu. Yeye yuko na atabaki kama gwiji wetu, lakini tafadhali Sadio, unataka kuondoka kwa sababu mahali pengine wanakulipa zaidi ni haki, lakini kuweka kisingizio cha watu wa Senegal...," **Beki wa zamani wa Liverpool, Jose Enrique akimkosoa Sadio Mane kutaka kuondoka Liverpool majira haya ya joto kwa madai kwamba watu wa Senegal wame mtaka kufanya hivyo.**



"Hii imekuwa miaka mitatu migumu, lakini mwakani nitatoa KILA KITU kwa ajili yenu nyie! Nina hakika mwaka ujao utakuwa wangu, sina shaka," **Mshambuliaji wa Real Madrid, Eden Hazard akieleza nia yake ya kusalia katika klabu hiyo msimu ujao.**



"Nitawakumbuka sana hawa wavulana. Nimekuwa hapa kwa miaka minane, lakini ninahisi kusudi langu limekamilika. Klabu iko katika mikono salama. Bado kuna mengi yanakuja kutoka kwa timu hii," **Mshambulizi wa Liverpool, Divock Origi ambaye anakaribia kuondoka Anfield msimu huu.**



# TETESI ZA USAJILI ZINAZOONGOZA KLABU LIGI KUU BARA



Straika hatari wa Vipers FC ya Uganda, Cesar Manzoki, ambaye ni mfungaji bora wa ligi ya huko, anayehusishwa na rada za Simba. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu nyingi duniani zimemalizika, huku Tanzania ikiwa ni moja kati ya nchi chache ambazo bado hazijamaliza ligi yake. Hata hivyo, tayari tetesi za usajili zimeshaanza duniani kote, huku baadhi ya timu zikiwa zimeshaandaa wachezaji wakuwasajili kwa ajili ya msimu ujao.

**Tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limeshatoa taarifa kwa timu zote wanachama kuwa mwisho wa usajili kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ni Juni 30, mwaka huu na hakutokuwa na nyongeza ya muda.**

Tanzania kama nchi zingine, pamoja na kwamba haijamaliza ligi yake, lakini tetesi za wachezaji kutoka nje ya nchi kuja kucheza soka la kulipwa tayari zimeanza. Lakini pia baadhi ya wachezaji kutoka klabu moja ya hapa kwenda nyingine nayo pia imeanza.

Kwenye makala haya tunakuletea wachezaji wa nje ya nchi na wa ndani ambao wamehusishwa kuwa watajiunga na klabu mbalimbali hapa nchini, twende sasa...

**#1. George Mpole - Geita Gold**

Ni straika ambaye yupo kwenye kiwango cha juu kwa sasa kwa kupachika mabao. Juzi aliifungia Taifa Stars bao kwenye mechi ya kutafuta tiketi ya kufuzu AFCON mwakani nchini Ivory Coast dhidi ya Niger.

Japo kuna taarifa kuwa ameongeza mkataba na timu yake, lakini timu kubwa za Simba, Yanga na Azam FC zimekuwa zikimtolea macho. Kwa sasa ana mabao 14 kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu sawa na Fiston Mayele wa Yanga.

Tetesi zinasema kuwa huenda akajiunga na moja kati ya timu hizo tatu kubwa. Pamoja na kuwa na mkataba na klabu yake, lakini timu za Simba na Yanga huwa hazishidwi kitu, linapokuja suala la usajili, hasa kwa mchezaji wa ndani.

**#2. Victorien Adebayor - US Gendamarie**

Huyu ni winga wa klabu ya US Gendamarie ya Niger, ambayo juzi alicheza dhidi ya Taifa Stars wakati Niger ikitoka sare ya bao 1-1 na Tanzania.

Ni winga machachari na alifanya vizuri kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika akiwa na timu yake hiyo. Anahusishwa mno kujiunga na klabu ya Simba, lakini pia ikidaiwa RS Berkane ya Morocco wameweka mzigo wa maana ili atue kwao.

Hata hivyo, mchezaji mwenyewe anaonekana kuwa na mapenzi na Simba, huku wakala wake akiwa na mapenzi na RS Berkane kutokana na kumuahidi pesa nyingi, iwapo dili hilo litakamilika.

**#3. Shiza Kichuya - Namungo**

Yupo kwenye kiwango kizuri msimu huu akiwa na timu yake ya Namungo, huku tetesi zikimhusisha kurejea kwenye klabu yake ya zamani, Simba.

Tetesi zinasema kuwa viongozi wa Simba wameamua kumrudisha ili hata kama wakiwa na winga mwingine kutoka nje wawe na kikosi kipana, ili kama akitoka mmoja, anayeingia awe anafanana na aliyetoka au kuwa na viwango visivyopishana sana.

**#4. Stephane Aziz Ki - Asec Mimosas**

Kiungo mshambuliaji huyu wa Klabu ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, raia wa Burkina Faso, awali alionekana kuwa kwenye rada za Simba.

Lakini baadaye ni kama viongozi wa Simba 'wakapotezea', na kwa sasa anatajwa kwenye tetesi za usajili ndani ya klabu ya Yanga. Naye pia alionekana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu yake ikiwa kundi moja na Simba.

**#5. Lazarous Kambole - Kaizer Chiefs**

Ni straika raia wa Zambia ambaye mkataba wake unamalizika kwenye klabu ya Kaizer Chiefs, huku akihusishwa kujiunga na klabu ya Yanga. Klabu hiyo inaonekana ni kama anaweza kuwa pacha wa Fiston Mayele, hasa kuelekea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

**#6. Nathaniel Chilambo - Ruvu Shooting**

Ni beki chipukizi ambaye yuko kwenye kiwango cha juu, akichezea Ruvu Shooting kwa sasa. Tayari klabu kubwa zimeshaanza kumzengea, ambapo awali Simba ilionekana kama vile ingeweza kumsajili kirahisi, lakini baadaye Azam FC inasemekana imeongeza mzigo na sasa ipo kwenye hatua nzuri ya kupata saini yake.

**#7. Cesar Manzoki - Vipers**

Ndiye mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwenye klabu ya Vipers ya Uganda, akiipa ubingwa pia timu hiyo. Raia huyu wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, anatajwa kuwa atavaa jezi nyekundu na nyeupe msimu ujao wa ligi akiwa na klabu ya Simba.

**#8. Pascal Wawa - Simba**

Ni mmoja wa wachezaji wanaodaiwa kuwa huenda watatemwa na klabu ya Simba mwishoni mwa msimu huu.

Tetesi zinasema kuwa klabu iliyopanda daraja msimu huu Singida Big Stars FC inamnyemelea raia huyu wa Ivory Coast na huenda akaitumikia msimu ujao wa Ligi Kuu.

**#9. Saido Ntibazonkiza - Yanga**

Siku chache tu baada ya kusimamishwa kwa utovu wa nidhamu, klabu ya Yanga pia ikatangaza kuachana na kiungo mshambuliaji huyo raia wa Burundi.

Klabu ya Singida Big Stars FC, ndiyo tetesi zinasema ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumnyakua pamoja na kwamba Azam FC nao wanamtolea macho.

**#10. Moses Phiri - Zanaco**

Ni straika raia za Zambia ambaye tetesi zinadai ameshamalizana na klabu ya Simba. Zipo tetesi zinasema kuwa Simba ilitaka kumsajili kipindi cha dirisha dogo, lakini klabu yake ya Zanaco iligoma, na kudai haitaweza kumtoa kutokana na kumtumia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Habari zinasema kuwa baada ya kumkosa, ilibidi wampe mkataba wa awali. Inaonekana ndiye chaguo namba moja kwa Simba msimu ujao wa ligi.

**JE, WAJUA?**



JUVENTUS ndiyo klabu iliyopoteza mara nyingi zaidi mchezo wa fainali wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kupokea kipigo mara tano, ikifuatiwa na Bayern Munich (mara 3), AC Milan (3), Liverpool (3) na Manchester United (2).





# 'Viongozi elimu fuateni miongozo TAMISEMI'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewataka viongozi wa elimu ngazi ya mikoa na halmashauri kusimamia na kufuata miongozo na taratibu zilizotolewa na ofisi hiyo.

Miongozo hiyo ni pamoja na namna ya kushughulikia kero mbalimbali za wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka 2022.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk. Charles Msonde, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa umma kuhusu maandalizi ya kufungua shule kwa wanafunzi wa kidato cha tano Juni 13, 2022.

Aliwataka wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka huu kufanya hivyo ndani ya wiki mbili na baada ya hapo atakayeshindwa kutimiza nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine.

Vile vile, alisema viongozi wa elimu mikoa, halmashauri na shule wanatakiwa kuhakikisha wanafunzi wanaandikishwa katika mfumo wa usajili wa wanafunzi wa sekondari (PReMS) na unatumika endapo wanahamishwa kwenda shule nyingine.

"Makatibu Tawala wa Mikoa wameshapatiwa mwongozo wa namna ya kushughulikia changamoto za uhamisho na ubadilishaji wa tahasusi ili wautumie kama rejea wakati wa kushughulikia changamoto mbalimbali za wazazi na wanafunzi," alisema.

Kadhalika, alisema ofisi hiyo inasisitiza kwa wale wote wenye matatizo waziwasilishe kwenye Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa ili zitatuliwe.

"Pia anaagiza mikoa kuhakikisha kuwa inalinda na kudhibiti idadi ya wanafunzi wanaohamishiwa katika shule ili kuepusha msongamano wa wanafunzi katika shule, pia kila mkoa utoe taarifa ya kuripoti kwa wanafunzi kila mwisho wa wiki kwa shule za serikali na Binafsi. Aidha, matumizi ya mfumo wa taarifa za shule (SIS) yazingatiwe ipasavyo," alisisitiza Dk. Msonde.

Vile vile, Dk. Msonde aliwaagiza Makatibu Tawala wa mikoa kuhakikisha wanadhibiti wanafunzi kutozwa michango ambayo haijaidhinishwa na mamlaka husika.

"Pia, viongozi wa elimu katika ngazi za mikoa na halmashauri kupitia maelekezo yaliyotolewa kwa wanafunzi kujiunga na shule yako sahihi na kuhakikisha kuwa wakuu wa shule wanatekeleza miongozo yote iliyotolewa na serikali kuhusu mapokezi, usajili na usimamizi wa shule," alisema.

Hata hivyo, Dk. Msonde alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa, vyoo, maabara na vituo vya walimu.

"Serikali imepeleka fedha nyingi na itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya elimu. Hivyo, ni wajibu wa kila kiongozi kuhakikisha kuwa, ujenzi unafanyika na kukamilika kwa wakati ili kutoa fursa pana zaidi ya upatikanaji wa elimu kama inavyotarajiwa," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songas Limited, Anael Samuel akizungumza na Spika wa Bunge, Tulia Ackson alipomtembelea Ofisini kwake Mjini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania kunufaika nishati mbadala kupikia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Ulaya (EU) kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, umeanzisha mradi wa nishati ya kupikia utakaogharimu Euro milioni 30 (sawa Sh. bil. 7.5) ili kuhamasisha jamii kutumia nishati mbadala.

Mwakilishi wa wizara hiyo, Emilian Nyanda aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya Wiki ya Mazingira inayofanyika jijini hapa.

Alisema Umoja huo pamoja na mashirika yake yanayojishughulisha na masuala ya mazingira unahamasisha jamii kuondokana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa kuwa inasababisha uharibifu wa mazingira.

Nyanda alisema mradi huo utakuwa ukisaidia mashirika binafsi na unatekelezwa katika mikoa mitano ikiwamo Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Pwani.

Awali, Mratibu na Mwakilishi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Clara Makenya, alisema UNEP kwa kushirikiana na mashirika mengine saba wamechukua hatua mbalimbali kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bioanuai na uchafuzi wa hali ya hewa.

Aidha, alisema wanaangalia namna watakavyoshirikiana na serikali kukabiliana na hali hiyo kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kupunguza mabadiliko ya tabianchi na athari za majanga.

Vilevile, alianisha vipengele saba vinavyozingatiwa kukabiliana na hali hiyo ambavyo ni kuwezesha kuwepo kwa takwimu zitakazotoa ushauri ili kuwapo usahihi kwa wafanya uamuzi, uwapo wa sera itakayoelekeza wadau namna Tanzania itakavyokabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, teknolojia kupunguza uharibifu.

"Kuwapo utafiti ili kutoa taarifa zinazoelekeza upande gani una changamoto ili hatua zichukuliwe kukabiliana na hali hiyo na kuwapo ushirikiano na wadau mbalimbali, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii kwa ujumla, tunahakikisha kila eneo lina kipengele kinachosaidia kukabiliana na changamoto hizo tatu za mazingira zinazoikabili Dunia," alisema Clara.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi unaochangia kuzuia athari za mabadiliko ya tabianchi wa shirika hilo, Aine Mushi, alisema shirika hilo limekuwa likihamasisha kuhusu matumizi ya nishati mbadala na wameanzisha mradi wa kuweka nishati hiyo katika Wilaya ya Chamwino, Kondoa na Mpwapwa.

# Waomba sera kukabiliana mabadiliko ya tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUKWAA la wachambuzi wa sera katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, limesisitiza umuhimu wa taifa kuwa na sera za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza athari zinazowakabili wakulima nchini.

Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Audax Rukonge, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya kongamano la nane la wadau wa kilimo.

Rukonge, alisema hali hiyo itasaidia kudhibiti mfumuko wa bei za vyakula kiholela na kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo na vitu vingine katika sekta hizo.

Alisema jukwaa hilo tangu mwaka 2013 limekuwa likiandaa makongamano ya kilimo ili kuwakutanisha wadau mbalimbali wa kilimo na kujadili changamoto zilizopo katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kutoa mapendekezo yao ya kisera.

"Hili ni kongamano la nane la wadau wa sekta ya kilimo kuhusu sera pamoja na kutathmini shughuli za kilimo nchini kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Kadhalika, alisema lengo la kongamano hilo mwaka huu ni kujadili athari za mabadiliko tabianchi ambavyo yameathiri sekta hizo nchini.

"Kazi yetu sisi ni kuchambua sera mbalimbali katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kuzitolea mapendekezo kwa serikali ili kuzifanyia maboresho na wananchi kunufaika katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi," alisema.

Naye, Mratibu wa Jukwaa hilo, Prof. David Nyange, alisema mada kuu katika kongamano la mwaka huu ni mabadiliko ya tabianchi yanavyo athiri sekta hizo.

"Mwaka huu tunakwenda kujadili namna ya kupunguza athari na kukabiliana na hayo mabadiliko tabianchi, mwaka huu mvua zilichelewa kumekuwepo na joto kali lakini mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na vita ya Urusi na Ukraine vimechangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa bei ya vyakula pamoja na pembejeo duniani," alisema.

Vilevile, alisema mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari nyingi ikiwamo ukame ambao unachangia kupungua kwa chakula, maji pamoja na malisho ya mifugo hali ambayo inasababisha jamii moja kuwa na migogoro na nyingine.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa lishe kutoka Shirika la uchambuzi wa sera za kilimo, Aspire Tanzania, Fortunata Chuwa, alisema mabadiliko tabianchi yamekuwa yakiathiri kwa kiasi kikubwa uhakika wa chakula na lishe nchini.

Mkuu wa kitengo cha usimamizi wa mazingira kutoka Wizara ya Kilimo, Prosper Makundi, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko tabianchi kupitia mkakati wake wa kitaifa.





## Kaya kufikiwa mfuko mawasiliano

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMLA ya kata 1,235 nchini zinatarajiwa kuunganishwa na huduma ya mfuko wa mawasiliano kwa wote (UCSAF) hadi kufikia Novemba mwaka huu, ili kuhakikisha huduma ya mawasiliano ya simu inapatikana kwa uhakika hasa maeneo ya vijijini.

Kwa mujibu wa Meneja wa UCSAF, mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Richard Sotery, juzi wakati wa semina kwa wamiliki wa vyombo vya habari na wanahabari jitihada hizo zinalenga kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana bila vikwazo vyovyote.

Mhandisi Sotery, alisema serikali kupitia mfuko wa UCSAF, unatoa ruzuku kwa watoa huduma ili waweze kufikisha mawasiliano ya simu, redio na televisheni kwa wananchi hasa kwa maeneo ambayo hayafikiki kirahisi.

"Katika kuhakikisha UCSAF tunaboresha huduma za mawasiliano kwa wote nchini, tumeingia makubaliano na watoa huduma kuzifikia kata 1,235 nchini kuziunganisha na huduma za mawasiliano hadi kufikia Novemba na kwamba kata 936 tayari zimeunganishwa na minara ya mawasiliano na zilizobaki utekelezaji wake unaendelea," alisema Mhandisi Sotery.

Akizungumzia maeneo ambayo yanapakana na nchi jirani, kupata tatizo la mawasiliano ya simu, redio kutokana na mwingiliano, Mhandisi Sotery alisema tayari jitihada zimeanza kuhakikisha wanaweka miundombinu imara ili kuzuia muingiliano na nchi nyingine.

Alisema mafunzo ya kuwajengea uwezo wanahabari yatasaidia kusambaza ujumbe juu ya shughuli zinazofanywa na mfuko huo na namna wanaweza kunufaika na mawasiliano kupitia mitandao ya simu, redio na televisheni.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwaomba wanahabari kuhabarisha umma juu ya shughuli zinazofanywa ili wananchi wapate taarifa sahihi za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mawasiliano.

Aidha, aliiomba UCSAF kuandaa mafunzo mengine ili kuwapiga msasa wanahabari namna bora ya kuandika vichwa vya habari ili kuwavutia wasomaji wa runinga za mitandao ambazo kwa sasa zimeshika kasi.

Patrick Kossima kutoka mkoani Ruvuma alisema mafunzo waliyoyapata ni juu ya namna mfuko wa mawasiliano kwa wote unavyofanya kazi ikiwamo namna ya kupata ruzuku kwa ajili ya kuboresha usikivu wa redio.

# Waja na mkakati kukomesha uvutaji sigara bila utaratibu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewaagiza wamiliki wa kumbi zote za starehe na maeneo ya mikusanyiko ya watu ikiwamo sokoni kutenga maeneo maalumu ya kuvutia sigara na tumbaku.

Aidha, mamlaka hiyo pia inakusudia kufanya uchunguzi wa kubaini aina ya vilevi au madawa ya kulevya yanayodaiwa kuchanganywa kwenye shisha baada ya kuonekana wavutaji wengi wa bidhaa hiyo wanalewa haraka ukilinganisha na sigara.

Hayo yalizungumzwa jana na Meneja wa TMDA, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, wakati wa mahojiano na Nipashe, kuhusu mkakati wao wa kuelimisha wananchi kuhusu matumizi ya tumbaku na sigara.

Alisema mikakati yao kwa mwaka huu ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari za matumizi ya sigara katika mwili wa binadamu sambamba na kusisitiza uvutaji wa kiistaarabu wa bidhaa hiyo ili kutokuwa kero kwa watu wengine wasiotumia.

"Wakati tunaadhimisha Siku ya sigara Duniani ifikapo Mei 31, tunapata nafasi ya kujadiliana kwa pamoja na kuweka mipango ya namna tunaokoa afya wa wananchi wetu kwa sababu uvutaji wa sigara ni miongoni mwa vichocheo vya magonjwa yasiyoambukizwa ikiwamo saratani ya koo, kizazi, magonjwa ya moyo, kifua na wakati mwingine kuharibu kabisa mfumo wa damu," alisema Mshighati.

Kutokana na athari mbalimbali za kiafya zitokanazo na uvutaji wa sigara aliwaasa watumiaji kuachana na matumizi ya bidhaa hiyo licha ya kuwa inachangia pato la taifa.

Alisema utoaji wa elimu kwa wananchi athari zitokanazo na tumbaku, utaanza Julai kwa kuzifikia kumbi zote za starehe zilizoko mikoa ya Nyanda za juu kusini, sambamba na kuhakikisha wanakuwa na maeneo maalum au vyumba kwa ajili ya kuvuta sigara au shisha hali kadhalika kwenye daladala na sokoni.

Aliongeza kuwa baada ya kumaliza utoaji elimu kwa wananchi, watafanya ukaguzi wa utekelezaji wake ikiwamo kuwachukulia hatua watakaokaidi maagizo hayo.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya akiwamo, Agripina Butusyo, aliipongeza TMDA kwa utaratibu huo kwa kuwa utasaidia kuondoa kero ya moshi wanaoupata katika maeneo ya starehe.

Alisema kumekuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa shisha kwenye kumbi za starehe na watumiaji wakubwa wa bidhaa hiyo ni vijana huku matokeo yake hulewa kupita kiasi na baadhi kupoteza kumbukumbu.

Alisema utaratibu wa kutengwa maeneo maalum ya kuvutia sigara utasaidia kuondoa kero kwa watu wengine wasiopenda harufu wala moshi wa bidhaa hizo.



Mwakilishi wa Jukwaa la Wadau wa Kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF) Owen Nelson, juzi akizungumza na wadau wa Kilimo, Maofisa Ugani kutoka Wilaya ya Mbeya, Kyela na Momba pamoja na Wakulima kutoka wilayani Kyela juu ya umuhimu wa matumizi ya Kilimo Ikolojia kwa ajili ya utunzaji wa mazingira na kutibu afya ya udongo ili kuzalisha kwa tija. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wataka sheria ya kilimo cha ikolojia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZALISHAJI wa mbolea za asili na wakulima katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wameiomba serikali kutunga sera itakayohamasisha matumizi ya kilimo Ikolojia ambayo itahamasisha matumizi ya mbolea hiyo katika uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini na kusaidia kutunza mazingira.

Wakulima na wadau wanaohusika na uzalishaji wa mazao mbalimbali walitoa rai hiyo jana, katika kikao hicho cha kujadili ni kwa namna gani kilimo cha Ikolojia kinaweza kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija na kuongeza rutuba katika udongo.

Mmoja wa wakulima hao, Tujolege Mwakisunga, kutoka kijiji cha Ndobo wilayani Kyela, alisema serikali itengeneze mifumo mizuri ya kuboresha kilimo cha ikolojia ambacho kina tija kwa mkulima kutokana na kufanya majaribio katika mashamba wa kilimo uliopita na kubaini kuongeza uzalishaji wa mazao mchanganyiko na kufufua ardhi iliyokufa kutokana na matumizi ya mbolea zenye sumu.

Mwakisunga alisema, mfumuko wa pembejeo za kilimo umewaibua wabunifu wa kuzalisha mbolea ya asili ya kutumia samadi na mabaki ya mpunga hivyo ni wakati sasa serikali kuunga mkono jitihada hizo ili kuongeza tija ya uzalishaji na kuwapo masoko ya uhakika ya ndani na nje.

"Msimu huu wa kilimo tumepata shida sana bei ya pembejeo ilipanda kupita kiasi, tunashukuru wataalam wakiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania TARI kwa kushirikiana na Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) walifanya utafiti wa udongo na kuhamasisha kilimo Ikolojia kinachohamasisha matumizi ya mbolea ya asili ili kuongeza uzalishaji wa mazao," alisema Mwakisunga.

Alisema kilimo cha Ikolojia kupitia mashamba darasa ya mpunga waliyoanzisha yameleta matumaini kwamba matumizi ya mbolea za asili yanaleta mavuno mengi na yenye ubora ukilinganisha matumizi ya mbolea za viwandani hivyo kutungwa kwa sera ya kuhamasisha matumizi ya mbolea asilia kwa kuzingatia kilimo Ikolojia ili kutunza mazingira kuleta tija.

Ofisa kilimo kata ya Mababu Wilaya ya Kyela, Benjamin Mwaijumba, alisema kuwa uwapo wa kilimo cha Ikolojia umeleta tija kwa wakulima kutokana na kuwapo kwa mfumuko wa gharama za pembejeo za kisasa.

"Tulifikiwa na kupatiwa elimu na watafiti wa Taasisi mbalimbali za Serikali na wakulima walipojaribu kilimo hicho wameona kina tija sana na pia kinachangia kufufua uhai wa ardhi ambayo imeharibiwa na matumizi ya mbolea zenye sumu," alisema.

Mtaalam wa mnyororo wa thamani wa mazao kutoka Jukwaa huru la wadau wa kilimo (Ansaf), Owen Nelson, alisema kuwa utafiti waliofanya katika sekta ya kilimo wamebaini uwapo wa manufaa makubwa kwa wakulima kutumia kilimo cha ikolojia kwa kutumia mbolea ya asili tofauti na za kisasa.

"Suala hapo ni wakulima kuzingatia elimu ya kitaalamu katika uzalishaji pia serikali ione umuhimu wa kuweka sera ya kuboresha kilimo cha ikolojia ili kutambulika ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa wazalishaji wa ndani," alisema.

Mwakilishi wa Ofisa Kilimo Mkoa wa Mbeya, Adam Mhagama, alisema changamoto ni maofisa ugani kutoa elimu ya matumizi ya pembejeo za kilimo za kisasa badala ya za asili ambazo ni nafuu kwa mkulima kutokana na mfumuko wa bei ya pembejeo nchini.

"Kilimo cha Ikolojia hakijapewa kipaumbele kwa maofisa ugani kukitangaza sasa kunahitajika nguvu ya ziada kuwashirikisha wanasiasa kuwafikishia elimu wakulima pamoja na vyombo vya habari kuhabarisha kupitia magazeti, televisheni na vipindi vya radio," alisema.



# ZIC yatoa mafunzo kwa Wawakilishi huduma 'Takaful'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Bima Zanzibar (ZIC) kwa kushirikiana na wadau wengine visiwani humo limeendesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa wajumbe wa Baraza la wawakilishi Zanzibar ikiwa ni moja ya hatua muhimu kuelekea utoaji wa huduma yake mpya ya Bima ya Kiislamu 'Takaful'.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyofanyika katika Baraza la Wawakilishi Chukwani nje kidogo ya jiji la Zanzibar, yalitanguliwa na mafunzo ya siku moja kwa mawakala wa bima visiwani humo yaliyofanyika Pemba huku lengo likiwa ni kuwaandaa wadau muhimu kuelekea kuanza matumizi ya bima ya kiislaam nchini.

Akizindua mafunzo hayo, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuleta mabadiliko katika kukuza huduma za bima ya kiislamu nchini huku akibainisha kuwa tayari nchi nyingi duniani zimeshafanya mabadiliko ya sheria za kifedha na kodi hivyo hatua hiyo itaweza kuweka mazingira bora ya kukuza na kustawisha huduma hizo.

"Ni imani yangu kuwa mfumo huu utaenda kuleta mabadiliko makubwa katika sekta za kibima hivyo ni wajibu wa serikali kuweka mikakati imara ili kuhakikisha wananchi walio wengi wananufaika," alisema.

Zubeir aliwataka Wajumbe wa Baraza hilo kuyatumia vyema mafunzo hayo ili kujijengea uelewa wakutosha pia waweze kupeleka uelewa huo kwa wananchi.

"Naamini pia kupitia uelewa huo mtaweza kuuliza maswali ya kina pamoja na kutoa maoni yenu muhimu kuhusu huduma hii ili wataalamu waweze kuyazingatia na kuyatekeleza kwa maslahi ya wananchi wetu hapa Zanzibar na taifa kwa ujumla," alisisitiza.

Vile vile, alitoa wito kwa mamlaka mbalimbali zinazohusika kufanikisha mpango huo zikiwamo taasisi za kifedha na mamlaka husika kufanya juhudi za kuruhusu utoaji wa huduma hiyo haraka iwezekanavyo pia kwa ufanisi unaotakiwa ili iwe na tija zaidi kwa wananchi wa kipato cha chini.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Arafat Haji alisema, kupitia mkakati wa uendeshaji wa mafunzo hayo shirika hilo linaamini kuwa taarifa muhimu kuhusu huduma hiyo mpya zitawafikia walengwa wote kote nchini ili kuichangamkia pindi itakapowafikia.

"Ni matumaini yetu kuwa ujio wa huduma hii ya Bima ya Kiislamu yaani 'Takaful' itakuwa ni suluhisho sahihi la kuwavutia wananchi wengi zaidi visiwani Zanzibar na maeneo mengine ya nchi ambao kimsingi wanahitaji huduma ya Bima ila wanashindwa kutokana na imani za kidini," alisema.

Alibainisha kuwa wananchi wengi wa visiwa vya Zanzibar wanasuasua kuingia katika mifumo ya bima kwa kujiepusha na riba ambazo zinaenda kinyume na silika na dini zao.

Akitoa shukrani zake kwa niaba ya serikali na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum pamoja na kuwapongeza wadau hao wakiwamo ZIC, alisema semina hiyo imeendeshwa kwa kundi muhimu kwa kuwa wajumbe hao wanawakilisha maelfu ya wananchi hatua itakayorahisisha usambazaji wa elimu hiyo.

"Baada ya mafunzo haya sisi kama viongozi wa serikali pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunabaki na jukumu kubwa la kuhakikisha elimu hii haibaki miongoni mwetu bali inawafikia wananchi tunaowawakilisha huko majimboni na hicho ndiyo kitu kinachofuata baada ya hapa. Huduma hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu na tutahakikisha inawafikia kama ilivyokusudiwa," alisisitiza.

Wadau wengine waliohusika katika utoaji wa mafunzo hayo kuhusu bima hiyo inayotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni ni pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Kituo cha Usimamizi wa Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri Tanzania (CIFCA) na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB).



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) Arafat Haji akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na wageni waalikwa wakati wa semina ya siku moja kwa wawakilishi hao iliyoendeshwa na shirika hilo kwa kushirikiana na wadau wengine visiwani humo ikilenga kuwajenga uelewa wajumbe hao kuelekea uanzishwaji wa huduma mpya ya Bima ya Kiislamu 'Takaful. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usafi mazingira hauhitaji siku maalum

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amewakumbusha wananchi suala la usafi wa mazingira halihitaji kutengewa siku maalum kwa kuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha maeneo wanayokaa mazingira yake yanakuwa safi na salama muda wote.

Aliyasema hayo jana baada ya kumaliza kufanya usafi wa mazingira katika Hospitali ya Wete akiwa na mwenyeji wake Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk, aliyeongozana na viongozi wa mkoa huo akiwamo Mkuu wa wilaya.

Waziri Harusi aliwasisitiza wanajamii kujenga utamaduni wa kudumisha usafi wakati wote hasa maeneo ambayo jamii inapata mahitaji ya kibinadamu kama hospitali, sokoni, sehemu za kazi kudumisha usafi kila baada ya muda ili kulinda afya zao wakati wote.

Kadhalika aliwakumbusha wananchi kuzingatia ujumbe wa Siku ya Mazingira Duniani ambao ni "Dunia hii ni moja" ukiwa na maana kutunza na kuhifadhi mazingira ni wajibu wa kila mtu na kinyume chake ni kuiharibu dunia kutokana na maumbile yake.

Pia, ameukabidhi uongozi wa Hospitali ya Wete mashuka 300 kwa wagonjwa yaliyotolewa na mfanyabiashara Suleiman Moh'd Anadi.

Wakati huo huo, Waziri Harusi, ameshirikiana na wanakikundi cha Tulianza Mapema kilichopo Tumbe Magharibi, kupanda miche ya mikoko eneo la bondeni ikiwa ni muendelezo wa kutunza na kuhifadhi mazingira hasa katika wiki ya maadhimisho ya sherehe ya siku ya mazingira duniani.

Aliwahakikishia wanakikundi hao kuwa serikali inaunga mkono juhudi za wananchi hasa wanaojitolea kulinda na kuhifadhi mazingira na kuwaomba wasivunjwe moyo na watu wachache wenye tamaa ambao wanavizia na kuikata mikoko na badala yake wote washirikiane kuwa walinzi wa mazingira ili kumshinda adui wa mazingira.

"Tunapaswa kuitunza miti ya mikoko kwa faida ya vizazi vijavyo na msichoke ili tuendelee kuvuta hewa safi na salama tuzidishe juhudi kulinda na kutunza mazingira na kurudisha uoto wa asili," alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa kikundi hicho Hamad Mwalimu Iddi alimuomba Waziri Harusi kusikia kilio chao na kupatiwa baadhi ya vifaa ili wajikinge na jua pamoja na boti ya doria kudhibiti baadhi ya watu wanaovizia kuikata mikoko.

Mkurugenzi Mtendaji wa Community Forest Pemba (CFP), Mbarouk Mussa Omar, alisema jumla ya miche 1,200,000 imepandwa kwenye eneo la Tumbe bondeni na kukipatia kikundi hicho Shilingi milioni tano za kusaidia shughuli na mahitaji ya kikundi.

Mbarouk alisema mazingira yanapoharibika viumbe vinaathirika, magonjwa yataongezeka, mvua zitapotea na kwamba ni wajibu wa wanajamii kuchukua juhudi za kupanda miti aina mbalimbali ili kurudisha uoto wa asili.

# Samia, Mwinyi wapongezwa utekelezaji anwani za makazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amewapongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa umakini wao wa utekelezaji wa anwani za makazi nchini.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, alieleza hayo wakati aliposhiriki uwekaji wa nambari za anwani za makazi katika Shehia ya Kiwengwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Waziri Dk. Khalid alisema dunia ipo katika maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, hakuna budi Tanzania nayo kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo hiyo ili kuwaunganisha wananchi wake na mifumo ya ulimwenguni.

"Umakini wa viongozi wetu hawa ndiyo umesababisha kupungua kwa gharama za kufanyika kwa zoezi hili kutoka Shillingi bilioni mia saba hadi kufikia bilioni ishirini na nane tu," alisema Dk. Khalid.

Alisema, kukamilika kwa anwani za makazi kutaliwezesha Shirika la Posta Tanzania pamoja na wadau wengine kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi.

Akitolea mfano wa mashirika makubwa duniani yanayofanya biashara kama Amazoni na Shirika la Alibaba, Dk. Khalid alisema wafanyabiashara wa Tanzania wataweza kuagiza bidhaa kutoka katika mashirika hayo na kufikishiwa hadi katika maeneo yao wanayoishi.

Waziri alisema Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kushirikiana na wizara nyingine zenye jukumu la zoezi la anwani za makazi zimefanya kazi nzuri ya uhamasishaji jambo ambalo kukamilika kwake kwa upande wa Zanzibar hakutokuwa na shaka.

Akilihusisha zoezi la anwani za makazi na Sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika nchini mwezi Agosti, mwaka huu, Waziri Dk. Khalid alisema, anuani za makazi (Post Code) limetandika njia ya urahisi katika kufanikisha sensa.

Naye, Sheha wa Shehia ya Kiwengwa, Masoud Ame alisema uongozi wa shehia hiyo umefanya kazi nzuri ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu zoezi linaloendelea jambo ambalo limesaidia kufanikisha kazi hiyo kufanyika vizuri.

Kwa upande wao watendaji wa zoezi hilo kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kasakazini, wameiomba jamii kuendelea kutoa ushirikiano wao katika kukamilisha zoezi hilo ambalo limefikia hatua ya uwekaji wa nambari katika nyumba ili zoezi likamilike kwa mujibu wa muda uliopangwa.

# Wanafunzi VETA walia na uhaba wa vifaa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) mkoani hapa, wameiomba serikali kuwapatia vifaa vya kutosha kwa ajili ya kujifunza masomo kwa njia ya vitendo.

Wamesema chuo hicho kina idadi kubwa ya wanafunzi, lakini kuna upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kulazimika kusoma kwa awamu darasani.

Wanafunzi walipaza kilio hicho mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya 38 ya chuo hicho.

Monica Ngowi alisema tatizo linalowakabili wanafunzi chuoni hapo ni upungufu wa vifaa vya kujifunzia.

"Chuoni hapa tupo wanafunzi 1,400, lakini vifaa havitoshi kwa ajili ya kujifunzia kwa njia ya vitendo, hivyo tunaiomba serikali itusaidie kupata vifaa vya kutosha, sababu sisi hapa chuoni masomo yetu hufanyika kwa vitendo zaidi," alisema Ngowi wakati akisoma risala.

Alitaja tatizo lingine ni upungufu wa vyumba vya madarasa, hosteli za wanafunzi, kituo cha afya kwa ajili ya matibabu ya wanafunzi, pamoja na ukosefu wa usafiri wa umma ambao utawafikisha chuoni.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Rashid Ntahigiye, alikiri kuwapo na tatizo hilo, na kuongeza ukosefu wa mfumo wa majitaka ambao husababisha kutumia gharama kubwa ya kukodisha magari kila wakati kusomba.

Kaimu Mratibu wa mafunzo chuoni hapo, Tajiri Mollel, alisema chuo hicho kina jumla ya wanafunzi 1,400 na kina uwezo wa kubeba wanafunzi 170 katika hosteli zao, huku akitaja idadi ya wanafunzi ambao wanahitimu kuwa ni 86, wavulana 44 na wasichana 42.

Kwa upande wake, mgeni rasmi kwenye mahafali hayo, Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliahidi serikali kushirikiana na chuo hicho kutatua baadhi ya matatizo yanayowakabili ili wanafunzi waendelee kupata ujuzi na kuwa faida kwa taifa hasa katika sekta ya ukuzaji wa viwanda.

Aliwataka pia vijana wanaohitimu VETA wachangamkie mikopo ya vijana inayopatikana halmashauri asilimia 10, ambayo asilimia nne hutolewa kwa vijana, nne wanawake na mbili watu wenye ulemavu, ili wapate mitaji na kujiajiri wenyewe kwa sababu wana ujuzi na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini (wapili kushoto) akitoka kutembelea ujenzi wa Jengo la Idara ya Uhamiaji mkoa wa Mtwara na kumwagiza mkandarasi kukamilisha ujenzi huo ndani ya mwezi mmoja na kwamba Serikali haijaridhishwa na kasi anayotumia katika hatua za kukamilisha ujenzi huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# TRA yatoa elimu ya mlipa kodi mlango kwa mlango

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeanza kampeni ya kutoa elimu kwa mlipa kodi kwa wafanyabiashara mkoani Shinyanga, ambayo itafanyika mlango kwa mlango ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari.

Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi kutoka TRA, Edwin Iwato, alibainisha hayo jana mkoani hapa wakati wakitambulisha kampeni hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema.

Alisema dira ya TRA ni kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ya ndani na kuwataka wafanyabiashara wawe wazalendo na nchi yao ikiwamo kulipa kodi kwa hiari bila kutumia mabavu.

"Kampeni hii ya elimu ya mlipakodi inayo julikana kama 'amsha amsha kampeni', tutaitoa ndani ya mwezi mmoja hapa mkoani Shinyanga kwa kutembelea wafanyabiashara wote mlango kwa mlango, kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari," alisema Iwato.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alitoa wito kwa wafanyabiashara mkoani humo kuwa na utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari ili serikali ipate fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mjema aliwasihi wafanyabiashara kuwa waaminifu wanapouza bidhaa zao kwa kutoa risiti, pamoja na wananchi wakinunua wadai risiti, jambo ambalo litafanikisha serikali kufikia malengo yake ya ukusanyaji mapato.

Katika hatua nyingine, Mjema alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kutoa ushirikiano na kushiriki kwa asilimia zote wakati wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti, 23 mwaka huu.

Alisema serikali ikiwa na idadi ya watu wake itakuwa rahisi kupanga mikakati yake na kuwatekelezea miradi mbalimbali ya maendeleo kulingana na uhitaji wao na kuwasihi siku hiyo wabaki nyumbani ili wahesabiwe.

# RC: Changamkieni fursa za mikopo

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAKAZI wa Mkoa wa Mwanza wametakiwa kuchangamkia fursa za uwekezaji na ufanyaji wa biashara ili kujiletea maendeleo ya kweli.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, katika hafla maalum iliyowakutanisha wateja wa Benki ya Akiba (ACB) jijini hapo.

Aliwataka wakazi hao kuchangamkia fursa ya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha itakayowasaidia kuanzisha biashara ili kukuza kipato chao.

Pia, vijana kuacha kulalamika kukosa mikopo badala yake wafuate maelekezo wanayopewa na taasisi hizo ili kukidhi vigezo.

Alisema ofisi yake ipo tayari kutoa maeneo ya bure kwa vijana na wawekezaji wenye mtaji ili kuwekeza katika sekta ya kilimo, ufugaji wa samaki wa vizimba na hoteli mkoani humo.

"Hata watumishi wa serikali, natoa rai kwenu kujitokeza kuchangamkia fursa ya mkopo unaotolewa, tusiishie kutegemea mishahara yetu bali tuongeze kipato kwa kuwekeza kwenye biashara na ACB imetuhakikishia kupata mikopo," alisema Gabriel.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Akiba (ACB), Sylvest Arumasi, alisema wanatoa mikopo ya biashara hadi Shilingi bilioni moja kwa wateja wake kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Alisema mbali na kutoa mkopo huo benki hiyo pia inatoa ushauri wa kibiashara kwa wateja wake ili kuwalinda dhidi ya hatari ya kupata hasara kwenye biashara zao.

"Ili kufanikisha hilo tumeanzisha ubia na Benki ya Taifa ya Malawi (NBM), ambao utasaidia kuboresha mazingira ya huduma za kifedha kwa ajili ya wateja hususani wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa," alisema Arumasi.

Kwa upande wake, mkazi wa Mkoa wa Mwanza, Remison Uiso, aliishukuru benki hiyo kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma kupitia internet banking huku akitoa wito kwa benki hiyo kutanua wigo hadi vijijini.

"Wananchi na wakazi wa kijijini wana uhitaji mkubwa wa huduma za mikopo na kuhifadhi fedha kinachowakwamisha ni kwamba huduma hizi zimejikita mjini, tanueni wigo hadi vijijini," alisema Uiso.

"Kuna watu wengine huko vijijini wanapoteza fedha kutokana na mazingira yasiyo rafiki ya uhifadhi wa fedha. Naamini mkifikisha huduma huko usalama wa fedha zao utaongezeka na uchumi wa nchi utaimarika."

# Korea Kaskazini yarusha makombora manane

**SEOUL,** Korea Kusini

JESHI la Korea Kusini limesema Korea Kaskazini imefyatua makombora manane ya masafa mafupi kuelekea pwani yake ya mashariki.

Korea Kaskazini imefanya jaribio hilo siku moja baada ya Korea Kusini na Marekani kukamilisha luteka ya pamoja ya kwanza ya kijeshi iliyohusisha ndege za kijeshi .

Muungano wa wakuu wa utumishi wa jeshi nchini humo ulisema jeshi lao limegundua makombora manane yaliyofyatuliwa kutoka eneo la Sunan nchini Korea Kaskazini kuelekea Bahari ya Mashariki jana. Kulingana na taarifa yao, zoezi hilo limefanyika kwa dakika 30 mapema.

Nchi hiyo imeendeleza mara dufu hatua zake za kuimarisha mipango ya silaha za nyuklia licha ya kukabiliwa na vikwazo vikali vya kiuchumi, kwa muda mrefu.

Korea Kaskazini imekuwa ikipinga luteka hizo za pamoja za kijeshi ikiziita kuwa ni mazoezi ya uvamizi.



Go Myong-hyuy, mtafiti kutoka taasisi ya masomo ya sera ya Asan ameliambia shirika la habari la AFP kwamba jaribio hilo la Korea Kaskazini huenda ni jibu kwa luteka hiyo ya kijeshi.

Waziri wa Ulinzi wa Japan, Nobuo Kishi (pichani) alisema hatua hiyo ya kufyatua makombora haitakiwi kuvumiliwa.

Mwezi uliopita, wakati wa mkutano wa kilele na Rais Yoon wa Korea Kusini, Rais Joe Biden wa Marekani aliahidi kupeleka vifaa vya kimkakati iwapo kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha ulinzi.

Marekani na Korea Kusini kwa wiki kadhaa sasa wamekuwa wakionya kuhusu nia ya Korea Kaskazini kufanya jaribio la kombora la nyuklia la masafa marefu ambalo ni la saba.

Licha ya kuelemewa na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya UVIKO-19 Korea Kaskazini imerejea kwenye ujenzi wa kinu cha nyuklia ambao ulisimama kwa muda mrefu, hii ikiwa ni kulingana na picha mpya za satelaiti. **DW**

# Rais Putin, atoa onyo kwa nchi za magharibi

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia Vladimir Putin, amezionya nchi za Magharibi kwamba vikosi vyake vitashambulia maeneo mapya ikiwa Marekani itaipatia Ukraine makombora ya masafa marefu.

Saa chache baada ya onyo hilo, jiji la Kyiv limeshuhudia mlipuko ulioambatana na mtikisiko, lakini haijafahamika ni shambulizi la aina gani.

Shirika la habari la TASS, lilimnukuu Rais Putin akisema kwamba watashambulia maeneo mengine lakini hakuyataja.

Ukraine imekuwa ikitafuta silaha za roketi ili kujibu mashambulizi kutoka kwa vikosi vya jeshi pamoja na hifadhi ya silaha ya Russia.

Rais wa Marekani Joe Biden mapema wiki hii alitangaza mipango ya kutoa mifumo ya roketi HIMARS baada ya kupokea uhakikisho kutoka Ukraine kuwa haitazitumia roketi hizo kulenga ndani ya Russia.

**Ukraine imekuwa ikitafuta silaha za roketi ili kujibu mashambulizi kutoka kwa vikosi vya jeshi pamoja na hifadhi ya silaha ya Russia.**

**MILIPUKO YATIKISA KYIV.**

Milipuko ilitikisa mji mkuu wa Ukraine Kyiv jana wakati gavana wa eneo hilo akielezea hali ya vita katika nchi yake.

Kupitia mtandao wa Telegram Meya Vitali Klitschko alisema hakuna waliofariki kutokana na mashambulizi ya makombora lakini mtu mmoja alijeruhiwa na alipelekwa hospitalini.

Rais Volodymyr Zelensky, alikiri hali katika mji wa Severodonetsk kuwa ni mbaya, ambapo mapigano ya mitaani yanaendelea.

Severodonetsk ni mji mkubwa zaidi ambao bado uko mikononi mwa Ukraine katika mkoa wa Luhansk katika jimbo la Donbas.

Vikosi vya Russia vimekuwa vikisonga mbele polepole katika wiki za hivi karibuni baada ya kurudi nyuma au kufukuzwa kutoka maeneo mengine.

**UKRAINE YAKASIRISHWA NA UFARANSA**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine Dmytro Kuleba amemkosoa Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kwa matamshi yake kuwa ilikuwa muhimu kwa Russia kutodhalilika.

Aidha, alisema ni muhimu kwa Rais Vladimir Putin kutafuta njia ya kutoka katika mzozo wa sasa katika kile alichokiita kosa la msingi alilolifanya.

Lakini Kuleba, alisema kuwa washirika wa nchi yake wanapaswa kujikita zaidi katika kuirejesha Russia kwenye njia sahihi.

Macron alikuwa akiwasiliana mara kwa mara na Putin kwa njia ya simu kama sehemu ya harakati za kumaliza mapigano na kufanya mazungumzo ya wazi. **BBC**



Majaribio ya Kombora Korea Kaskazini. **PICHA:DW**

# Mlipuko waua watu 40 Bangladesh

**DHAKA,** Bangladesh

MLIPUKO ulioambatana na moto mkubwa uliotokea katika ghala moja umesababisha vifo vya watu 40, na mamia kujeruhiwa.

Ghala lilotokea ajali hiyo liko karibu na mji wa Chittagong, nchini Bangladesh.

Mamia ya watu walifika kukabiliana na moto huo wakati makontena kadhaa yalipolipuka katika eneo la Sitakunda.

Chanzo cha moto huo hakijajulikana, lakini inadhaniwa kemikali zilihifadhiwa katika baadhi ya makontena hayo.

Hospitali katika eneo hilo zimezidiwa na majeruhi na zimeomba msaada wa kuchangiwa damu.

Idadi kubwa ya waliojeruhiwa wanaripotiwa kuwa katika hali mbaya huku majeraha ya moto yakichukua asilimia 60 hadi 90 ya miili yao.

“Mlipuko huo ulinirusha umbali wa mita 10 kutoka mahali nilipokuwa nimesimama. Mikono na miguu yangu imeungua,” alisema dereva wa lori Tofael Ahmed wakati akiongea na shirika la habari la AFP.

Mhudumu mwingine wa kujitolea aliliambia shirika hilo kuwa ameona miili zaidi ndani ya eneo lililoathiriwa na moto huo.

Wazima moto kadhaa ni miongoni mwa waliouawa na kujeruhiwa.

Bohari hiyo ilikuwa na nguo za mamilioni ya dola zilizokuwa zikisubiri kusafirishwa kwa wauzaji reja reja wa nchi za Magharibi, kulingana na afisa wa serikali ya eneo hilo.

Bangladesh ni muuzaji mkuu wa nguo kwa nchi za Magharibi. **DW**

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA KAMBINI KUIWINDA NAMUNGO FC

Na Saada Akida

KIKOSI cha timu ya Polisi Tanzania kimeanza kambi ya siku 10 katika Shule ya Maofisa wa Polisi Kurasini, Dar es Salaam kikijiwinda na michezo miwili ya Ligi Kuu iliyopo mbele yao dhidi ya Namungo FC na Yanga.

**Juni 16, mwaka huu Polisi Tanzania watashuka uwanjani ugenini dhidi ya Namungo FC katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Ilulu, Lindi saa 10 alasiri.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema baada ya kumalizika kwa michezo miwili ya Ligi Kuu nyumbani dhidi ya Mtibwa Sugar na Biashara United, wachezaji walipewa mapumziko ya wiki moja ambayo yamemalizika juzi na jana kuingia kambini.

Alisema kutokana na umuhimu wa michezo hii, miwili katika kusaka alama tatu, uongozi umeona ni vema kuweka kambi eneo ambalo hali ya hewa yake haitofautiani na Lindi.

"Timu itapata utulivu wa kutosha na tunaendelea na maandalizi kuhakikisha tunavuna pointi tatu dhidi ya wenyeji wetu, tunatambua ubora wa Namungo FC na tutaenda kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri kwa kuvuna pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo kwa inaelekea ukiongoni kwa ushindani mkali zaidi hasa kwa kuzingatia anayepoteza mechi hushuka nafasi moja na anayeshinda kupanda juu.

Polisi Tanzania ipo nafasi ya saba katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa imejikusanyia alama 33 baada ya kucheza michezo 26 na imesaliwa na mechi nne dhidi ya Namungo, Yanga, GeitaGold na Kagera Sugar.

Katika michezo hiyo, miwili watacheza ugenini huku dhidi ya Geita Gold FC na Polisi Tanzania watakuwa nyumbani katika uwanja wao wa Ushirika mjini Moshi.

MAPEMA TU...



Wachezaji wa Taifa Stars wakimpongeza George Mpole baada ya kuifungia bao la kuongoza katika dakika ya kwanza ya mchezo wa kuwania kufuzu Afcon 2023 dhidi ya Niger iliyopigwa Uwanja wa Stade de l'Amitie, Cotonou nchini Benin juzi na timu hizo kutoshana nguvu kwa kufungana 1-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *JKT Tanzania mguu mmoja Ligi Kuu*

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Maafande wa Jeshi la Kujenga Taifa, JKT Tanzania, wameonyesha azma yao ya kutaka kurejea tena Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya juzi kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Kitayosce kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, ikiwa ni mechi ya mkondo wa pili ya mchujo, Ligi ya Championship.

Kwa matokeo hayo, JKT Tanzania imepita hatua hiyo kwa jumla ya mabao 3-1, kutokana na mechi ya kwanza iliyochezwa hivi karibuni katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, kushinda kwa mabao 2-0.

Timu hiyo ambayo ilishuka daraja msimu wa 2019/20, kwa sasa inasubiri kucheza na mshindi wa timu za Ligi Kuu ambazo zitamaliza zikiwa kwenye nafasi ya 13 na 14.

Zitakazomaliza nafasi hizo zitacheza mechi ya mchujo na itakayoshinda ndiyo itacheza dhidi ya JKT Tanzania kutafuta timu itakayocheza Ligi Kuu, au Championship.

Iwapo maafande hao watashinda, basi watapanda kucheza Ligi Kuu, lakini kama wakifungwa watabaki kwenye Ligi ya Championship, huku timu ya Ligi Kuu ikishinda itabaki huko huko, lakini ikipoteza itashuka daraja na kucheza Championship msimu ujao.

Timu za Ndanda na Pan African nazo zimefanikiwa kubaki kwenye Ligi ya Championship, baada ya kushinda mechi zao za mchujo juzi.

Ndanda ikiwa Nangwanda Sijaona, iliichapa Gwambina mabao 2-0 na kulazimika kupigiana penalti kwani mechi ya kwanza pia Gwambina ilishinda mabao 2-0, Ndanda ikabaki kwa kushinda kwa mikwaju 2-1.

Pan African ugenini, Mkwakwani Tanga, nayo ilifanikiwa kubaki kwa kufungwa African Sports kwa mikwaju 5-3, baada ya kila timu kushinda mabao 2-0 nyumbani kwake.

# Coastal yapania kumaliza 4-bora

Na Cheji Bakari, TANGA

LICHA ya kukabiliwa na mchezo mgumu ujao dhidi ya vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga, uongozi wa Klabu ya Coastal Union umesema malengo yao ni kushinda mechi zao zote nne zilizosalia ili kufikia malengo ya kumaliza nafasi nne za juu katika ligi hiyo .

Juni 15, Coastal Union itakuwa ugenini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuvaana na vinara wa Ligi Kuu, Yanga ambao wanahitaji pointi tatu tu katika mechi zao nne zilizosalia ili kutawazwa mabingwa wa msimu huu wa 2021/22.

Coastal Union ambayo ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kucheza michezo 26 na kujikusanyia jumla ya alama 34, imebakisha mechi nne kabla ya msimu kumalizika, mbili zikiwa za ugenini dhidi ya Yanga na kisha Namungo Juni 18.

Baada ya hapo timu hiyo itarudi nyumbani katika uwanja wake wa Mkwakwani kucheza na Kagera Sugar kwenye mechi ya mzunguko wa 29 kabla ya Juni 19 kumaliza Ligi Kuu kwa kucheza na Geita Gold FC uwanjani hapo.

Akizungumza na gazeti hili msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi, alisema uongozi mzima wa Coastal Union unataka kuhakikisha unashinda mechi zote nne zilizobaki ili kumaliza katika nafasi nne za juu katika msimamo wa Ligi Kuu.

"Nikuhakikishie kuwa uongozi mzima wa Coastal Union kuanzia Kamati Tendaji chini ya Mwenyekiti Steven Mnguto, Kamati ya Mashindano, mashabiki na matawi watahakikisha Coastal Union inashinda mechi zote zilizobaki, ikitokea bahati mbaya labda suluhu, lakini hatutaki kufungwa," alisema.

Aliongeza: "Kuhusu bonasi walizoahidiwa wachezaji tunashukuru uongozi umetekeleza ahadi zake, wachezaji wamepata pesa zao".

Ligi hiyo kwa sasa imesimama kupisha mechi za Kalenda ya Fifa, zinazoendelea ambapo kwa bara la Afrika ni kuwania kufuzu fainaliza Afcon 2023 zitakazofanyika nchini Ivory Coast.

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN HUYOOO UNITED

KLABU ya Manchester United ina matumaini kwamba, inaweza kumnasa mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen kwa uhamisho huru baada ya mkataba wake wa muda mfupi pale Brentford kumalizika mwishoni mwa Juni. ***(Mirror)***

### ARSENAL YAMWAMULIA JESUS



ARSENAL wako tayari kumpa mshambuliaji wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25, mshahara pauni 190,000 kwa wiki ili kuhamia pale Uwanja wa Emirates msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### MANE KUONDOKA ANFIELD

SADIO Mane amesisitiza kuwa anataka kuondoka, huku mshambuliaji huyo akihusishwa na Bayern Munich, akikaa kimya bila kudai chochote kuhusu mkataba mpya pale Anfield. ***(Daily Telegraph)***

### DEMBELE KUTUA CHELSEA




CHELSEA wanaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsaka mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele, ambaye atapatikana bure baada ya mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, utakapokamilika mwishoni mwa mwezi huu. ***(Talksports)***

### MOUNRIHO AMPIKU ZIDANE

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho mwenye umri wa miaka 59 ameibuka kuwa mpinzani wa Zinedine Zidane kuwania nafasi ya Mauricio Pochettino kama kocha mpya ajae wa Paris St-Germain. ***(Daily Mail)***

### AGOMBEWA ENGLAND



TOTTENHAM Hotspur, Newcastle na Aston Villa zote zinamtaka winga wa Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye umri wa miaka 28 kutoka Atletico Madrid. ***(Fichajes)***

### PULISIC KWA VIGOGO ITALIA

AC Milan na Juventus zinamfuatilia winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 23, Christian Pulisic, ambaye hafurahishwi na kusugua benchi pale Stamford Bridge. ***(Daily Mail)***

### MAXIMIN AWINDWA SPURS



TOTTENHAM Hotspur wanavutiwa na mshambuliaji wa Newcastle mwenye umri wa miaka 25, Allan Saint-Maximin. ***(Football London)***

### AKE NA NEWCASTLE UNITED

NEWCASTLE itahitaji kulipa pauni milioni 50 ili kumsajili beki wa Manchester City, Nathan Ake mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### PALACE KWA ARIBO



KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Rangers na Nigeria, Joe Aribo mwenye umri wa miaka 25. ***(The Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LIVERPOOL SASA YAJITOSA MAZIMA KWA RAPHINHA

### ●●● Takumi Minamino anaweza kutumika kama sehemu ya kumsajili nyota huyo ambaye alichangia...

**LONDON,** England

HUKU kuondoka kwa Sadio Mane kukiwa karibu kutimia, Liverpool wameamua kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya winga wa Leeds United, Raphinha, kwa mujibu wa Mirror.

Raphinha amekuwa akitajwa zaidi kuwaniwa kule Barcelona na inadaiwa kwamba, wakati wowote anaweza kutangazwa kuwa nyota mpya wa miamba hao wa kule kwenye viunga vya Katalunya.

Baada ya kupoteza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, hitaji lao kubwa kwa sasa ni kutaka kujenga upya kikosi cha Liverpool, huku wachezaji kadhaa wakitajwa kuwaniwa.

> **Uhamisho wa Luis Diaz wakati wa dirisha dogo la Januari ulitoa kipengele kipya katika uchezaji wa Liverpool chini ya kocha, Jurgen Klopp, huku kuondoka kwa Mane kukiwaacha kwenye wakati mgumu.**

Raphinha mchezaji wa kimataifa wa Brazil kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na Barcelona, lakini matatizo yao ya kifedha ambayo yanatangazwa sana, yanawahitaji kuuza wachezaji wengine kabla ya kusajili.

Takumi Minamino wa Liverpool anaweza kutumika kama sehemu ya kumsajili Raphinha mwenye umri wa miaka 25, ambaye alichangia pasi 11 za mabao wakati Leeds ikibaki kwenye Ligi Kuu England.

Kocha wa Leeds, Jesse Marsch anaripotiwa kuwa shabiki mkubwa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Japan, na hivyo kuwaacha Liverpool wakiwa na uwezekano mkubwa wa kufanikisha dili hilo.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
CROATIA
VERSUS
FRANCE
1 | 3.64
X | 3.39
2 | 2.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO ATAKIWA PSG KUMRITHI POCHETTINO



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain ina nia ya kumfanya Jose Mourinho kuwa kocha wake mpya huku wakijiandaa kumalizana na Mauricio Pochettino, kwa mujibu wa 90min.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa muda mrefu wamekuwa na mipango ya kumtoa Pochettino mwishoni mwa msimu huu na walikuwa wakitaka kumbadilisha na kumchukua Antonio Conte, ambaye yuko kule Tottenham Hotspur.

Huku wakimtaka kocha mpya, PSG pia wanakaribia kumuajiri Luis Campos kama mkurugenzi wao mpya wa michezo, na kwa mujibu wa 90min, mkuu huyo wa zamani wa Lille na Monaco anaangalia chaguzi zake anapojiandaa kukata uhusiano na Pochettino.

Wawakilishi wanaofanya kazi kwa niaba ya PSG wamewasiliana na Mourinho ili kupima nia yake ya kuchukua kazi hiyo, huku upande wa Ligue 1 ukivutiwa na matarajio ya kufanya kazi na kocha huyo wa AS Roma.

Mourinho anajulikana kuwa karibu na Campos, ambaye alifanya kazi chini yake kule Real Madrid, na bosi huyo alishindwa katika jaribio la kumleta raia mwenzake huyo wa Ureno pale Manchester United.

Mourinho inasemekana kufurahishwa sana na Roma na hata amesema hadharani kwamba hana mpango wa kuwaacha mabingwa hao wa Ligi ya Europa Conference.

"Ninaziheshimu sana klabu zote ambazo nilifanya nazo kazi, lakini leo mimi ni 'Romanista' kwa asilimia 100, kwa sababu mashabiki hawa ni wa kushangaza," alisema baada ya ushindi wa taji la Europa Conference.

"Nitabaki AS Roma, bila shaka, hata kama ofa zitakuja. Nataka kubaki hapa."

Licha ya Mourinho, Campos pia anadaiwa kutaka kufanya kazi na kocha wa Nice, Christophe Galtier na yule wa Monaco, Leonardo Jardim.

Hata hivyo, inadaiwa kwamba, kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim ndiye mwenye nafasi kubwa zaidi ya kuchukua mikoba ya kuwa pale PSG msimu ujao.



## *Mane aweka rekodi Senegal*

**DAKAR,** Senegal

SADIO Mane amekuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Senegal baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati wakipata ushindi wa 3-1 dhidi ya Benin katika mchezo wao wa kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, Jumamosi.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool, alifunga mara mbili kwa penalti na kufunga jingine mjini Dakar, hivyo kufikisha mabao 32 katika mechi 90 alizoichezea nchi yake.

Mabao hayo matatu ya Mane yalimuweka mbele ya Henri Camara mwenye mabao 31 kwa mabingwa hao wa Afrika.

Mafanikio ya kuvunja rekodi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, yanakuja huku kukiwa na uvumi mkubwa juu ya hatima yake baada ya msimu mwingine bora kwa kikosi cha kocha, Jurgen Klopp pale Liverpool.

Ijumaa, mshambuliaji huyo alidai kwamba, atafanya kile ambacho watu wake wa Senegal wanataka afanye, huku kukiwa na ripoti kwamba, anaweza kuwa njiani kuelekea Bayern Munich.

Wananchi wa Senegal walipiga kura kwenye gazeti moja nchini humo kumtaka Mane aondoke Liverpool kipindi hiki cha majira ya joto.

Asilimia 60 hadi 70 ya waliopiga kura walitaka Mane akacheza kwenye timu nyingine msimu ujao.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# SAMATTA AWAITA MASHABIKI KWA MKAPA 'KUIUA' ALGERIA

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kuambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya Niger kwenye mechi ya kwanza ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast, Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, amesema ingawa itakuwa mechi ngumu dhidi ya Algeria keshokutwa Jumatano, lakini wanahitaji ushindi.

Ikiwa katika Uwanja wa l'Amitie, Cotonou nchini Benin juzi, Stars ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Niger ambao ilitumia dimba hilo kutokana na viwanja vyake kutokidhi ubora.

Katika mechi inayofuata, Stars sasa itaikaribisha Algeria katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano, ambayo imetoka kushinda mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Uganda.

Akizungumzia mchezo huo dhidi ya Algeria, Samatta alisema utakuwa mgumu kwa kuwa aina ya mpinzani wanayekutana naye ni moja kati ya timu bora zaidi katika viwango vya soka Afrika, lakini kwa kuwa watakuwa nyumbani watapambana kupata matokeo.

"Kuhusu mchezo unaofuata, nadhani utakuwa mgumu na tunafahamu mpinzani tunayekwenda kukutana naye katika viwango vya Afrika ni namba moja ama mbili kimichezo, nafikiri utakuwa mgumu, lakini ni mchezo wetu wa kwanza nyumbani tunahitaji pointi tatu.

"Tutapambana kwa hali na mali, hivyo Watanzania waje kwa wingi tuweze kusapotiana kwa sababu tunataka pointi tatu nyumbani," alisema Samatta anayeichezea Klabu ya Antwerp ya Ubelgiji kwa mkopo akitokea Fenerbahçe ya Uturuki.

Kuhusu mechi dhidi ya Niger, Samatta alisema kwa ujumla ulikuwa mchezo mgumu katika nyanja nyingi na kwamba wangeweza kupata matokeo zaidi ya droo waliyoipata, lakini hata hivyo anaamini pointi moja waliyoipata itakuwa muhimu katika muendelezo wao kwenye mechi za kufuzu fainali hizo.



Stars ambayo ilitarajiwa kurejea jana ikitokea Benin itareja mazoezini kesho kujianda mechi hiyo, ambayo inatarajiwa kuwa ngumu zaidi katika kundi lao.

Ikumbukwe timu mbili zitakazomaliza nafasi ya juu katika kila kundi, ndizo zitakzofuzu kushiriki fainali hizo nchini Ivory Coast mwakani.

# Udoh atajwa kuja Simba kurithi viatu vya Lwanga

Na Mwandishi Wetu

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara wakieleza kwamba wanataka kukisuka upya kikosi chao kwa kusajili nyota wa kiwango cha juu mwenye kiu ya mafanikio kuelekea msimu mpya, wamehusishwa kutaka kumsajili Kiungo Mnigeria, Udoh Etop David.

Rais wa Heshima na Mwekezaji, wa klabu hiyo, Dk. Mohamed 'Mo' Dewji, wiki iliyopita alisema wanataka kusafisha na kuunda upya kikosi chao kwa kusajili nyota wa kiwango cha juu wenye uchu wa mafanikio wakati huu wakielekea kumaliza msimu na Kombe la Mapinduzi pekee.

Hata hivyo, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, baada ya kuulizwa ni nyota gani ambao wapo kwenye rada za kusajiliwa na klabu hiyo, alisema kila kitu kitajulikana baada ya msimu kumalizika, lakini tetesi zinaeleza, Udoh ni miongoni mwa nyota wanaowindwa na miamba hiyo.

Ikumbukwe Udoh, aliwahi kufanya majaribio na klabu hiyo na kuichezea katika michuano ya Kombe la Mapinduzi msimu huu, lakini hakukidhi matakwa ya benchi la ufundi lililokuwa chini ya Mhispani Pablo Franco.

Lakini sasa Udoh anahusishwa kuja kuridhi viatu vya Mganda Taddeo Lwanga ambaye klabu hiyo imepanga kuachana naye mwishoni mwa msimu kutokana na historia yake ya majeraha ya mara kwa mara.

Simba ambayo msimu huu imeishia hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, huku ikishika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa nyuma kwa alama 13 dhidi ya vinara Yanga wenye pointi 64, ni wazi 'Wekundu' hao wataambulia Kombe la Mapinduzi pekee kwa msimu huu kwani tayari wameshatolewa kwenye kinyang'anyiro cha Kombe la FA.



MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 06/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1913 | Hoganas BK vs Torslanda IK | 3.64 | 3.79 | 1.78 |
| 14:00 | 2044 | South Korea vs Chile | 2.21 | 3.21 | 3.37 |
| 14:00 | 2700 | Traeff vs Ullensaker/Kisa | 4.52 | 4.33 | 1.54 |
| 14:00 | 2807 | Alta IF vs Frigg | 1.57 | 4.32 | 4.32 |
| 14:00 | 2809 | VRI vs Norresundby BK | 1.98 | 3.83 | 2.99 |
| 14:00 | 3312 | Levanger vs Hodd | 2.95 | 3.59 | 2.07 |
| 15:00 | 4137 | Japan U22 vs Colombia Youth | 3.09 | 3.18 | 2.16 |
| 15:00 | 4273 | Egersund IK vs Notodden | 1.34 | 5.10 | 6.27 |
| 15:00 | 4428 | Odder Igf vs Ringkobing IF | 2.03 | 3.74 | 2.95 |
| 15:00 | 5467 | Volda vs Lillehammer FK | 1.65 | 4.42 | 3.73 |
| 15:00 | 5980 | FC Einheit Wernigerode vs Einheit Rudolstadt | 1.81 | 3.83 | 3.49 |
| 16:00 | 1380 | SV 1914 Eilendorf vs SV Deutz 05 | 1.21 | 6.47 | 8.63 |
| 16:00 | 1584 | Kvik Halden vs Sotra | 1.57 | 4.30 | 4.30 |
| 16:00 | 2326 | Honefoss vs Forde | 1.93 | 4.23 | 2.90 |
| 16:00 | 2561 | Viktoria Arnoldsweiler vs VfL Alfter | 2.60 | 4.40 | 2.16 |
| 16:00 | 3436 | Vindbjart vs Sarpsborg Sparta 2 | 1.80 | 4.42 | 3.15 |
| 16:00 | 3850 | SV 1910 Breinig vs VfL Vichttal | 8.87 | 5.91 | 1.22 |
| 16:00 | 4147 | Bor. Freialdenhoven vs Hennef 05 | 3.14 | 4.32 | 1.82 |
| 16:00 | 4723 | Japan U23 vs Saudi Arabia U23 | 2.44 | 3.08 | 2.74 |
| 16:00 | 4726 | Bergisch Gladbach vs 1. FC Duren | 2.47 | 4.10 | 2.31 |
| 16:00 | 4883 | Eidsvold Turn vs Asker | 2.28 | 3.62 | 2.59 |
| 16:00 | 5882 | Eik-Tonsberg vs Halsen IF | 1.40 | 5.11 | 5.31 |
| 16:30 | 1370 | Spvg Frechen 20 vs FC Hurth | 1.63 | 4.40 | 4.20 |
| 16:30 | 5362 | Siegburger SV 04 vs FC Pesch | 2.05 | 4.20 | 2.85 |
| 17:00 | 1350 | Strindheim IL vs Trygg/Lade | 1.24 | 6.10 | 7.68 |
| 17:00 | 1683 | Gjellerasen vs Floya | 1.64 | 4.32 | 3.88 |
| 17:00 | 3624 | Baerum vs Kjelsaas | 3.09 | 3.63 | 2.00 |
| 17:00 | 4117 | Odds BK 2 vs Moss | 3.33 | 3.72 | 1.88 |
| 17:00 | 4464 | Harstad vs Mjondalen 2 | 3.10 | 4.33 | 1.83 |
| 17:00 | 4621 | Start 2 vs Mandalskameratene | 3.09 | 4.02 | 1.89 |
| 17:00 | 4869 | Orn-Horten vs Strommen | 2.42 | 3.48 | 2.50 |
| 18:30 | 2522 | TPS Turku vs PK-35 | 1.50 | 3.88 | 5.69 |
| 20:00 | 1552 | Mbour Petite Cote vs ASC Jaraaf | 5.29 | 2.94 | 1.75 |
| 20:00 | 1921 | US Goree vs AS Douanes | 2.66 | 2.56 | 3.00 |
| 20:00 | 2100 | AS Dakar Sacre Coeur vs Generation Foot | 3.75 | 2.70 | 2.25 |
| 20:00 | 3105 | Teungueth vs Casa Sport | 2.75 | 2.55 | 2.90 |
| 20:00 | 5143 | Cneps vs ASC Diambars | 1.97 | 3.24 | 3.54 |
| 20:00 | 5536 | Asec Ndiambour vs AS Pikine | 3.09 | 2.55 | 2.60 |
| 21:30 | 2076 | Justo Jose De Urquiza vs Villa San Carlos | 2.70 | 2.65 | 2.84 |
| 21:30 | 4138 | Deportivo Riestra vs Deportivo Madryn | 2.21 | 2.81 | 3.45 |
| 21:30 | 5408 | Deportivo Muniz vs Argentino Rosario | 2.80 | 2.80 | 2.60 |
| 21:30 | 5623 | Deportivo Paraguayo vs Central Ballester | 3.68 | 2.80 | 2.12 |
| 21:45 | 1618 | Slovakia vs Kazakhstan | 1.27 | 5.23 | 11.07 |
| 21:45 | 3619 | Andorra vs Moldova | 3.58 | 3.13 | 2.12 |
| 21:45 | 4019 | Austria vs Denmark | 2.82 | 3.27 | 2.44 |
| 21:45 | 4256 | Belarus vs Azerbaijan | 2.77 | 2.92 | 2.72 |
| 21:45 | 4607 | Iceland vs Albania | 2.47 | 3.08 | 2.93 |
| 21:45 | 4805 | Croatia vs France | 3.64 | 3.39 | 2.00 |
| 22:00 | 2935 | Equatorial Guinea vs Libya | 2.05 | 3.12 | 3.82 |
| 23:00 | 1646 | Bonaire vs Sint Maarten | 1.11 | 7.48 | 14.77 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Juni 6, 2022
Nipashe




Liverpool yajitosa kwa Raphinha UKURASA 21

TAYARI HUKO...



George Mpole (kulia) akishangilia na wachezaji wenzake wa Taifa Stars baada ya kuifungia bao la kuongoza katika dakika ya kwanza ya mchezo wa kuwania kufuzu Afcon 2023 dhidi ya Niger uliopigwa Uwanja wa Stade de l'Amitie, Cotonou nchini Benin juzi na timu hizo kutoshana nguvu kwa kufungana 1-1. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Poulsen alia Stars kucheza na Niger 12

## ●●● Ni wakati ikitoka sare Benin kuwania kufuzu Afcon 2023, asema kama isingekuwa...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Kim Poulsen amesema wachezaji wake walikuwa wakicheza na wapinzani 12, kwani mwamuzi wa mchezo huo alikuwa akiwabeba kwa mbeleko Niger.

Akizungumza baada ya kutua jana nchini Tanzania wakitokea nchini Benin kucheza mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya michuano ya AFCON inayotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Ivory Coast, kocha huyo alisema mechi ilikuwa ngumu uwanjani, lakini pia mwamuzi alionekana kuwabeba wapinzani wao, hivyo ni kama walikuwa wakicheza na wachezaji 12.

"Ilikuwa mechi ngumu, kipindi cha kwanza tulifunga, wao wakarudisha, kipindi cha pili tulikosa nafasi kadhaa za kufunga ambazo zingetupa pointi tatu, lakini ifike wakati tushukuru hata pointi hii moja tuliyoipata ugenini.

Ilikuwa pia mechi ngumu kwa sababu waamuzi walikuwa wakiwabeba wapinzani wetu, ni kama tulikuwa tunacheza na wachezaji 12 muda wote, kila maamuzi yalikuwa ni ya kutukandamiza, ni kama vile alikuwa na ajenda ya kutupa kadi nyekundu. Hiki si kitu kizuri kwenye soka, lakini mwisho wa siku mechi imeisha kwa sare," alisema kocha huyo.

Stars ndiyo iliyoanza kutangulia kupata bao kwenye Uwanja wa l'Amitie, Cotonou nchini Benin lililowekwa wavuni na straika anayekuja juu kwa sasa, George Mpole dakika ya kwanza, wapinzani wakisawazisha kupitia Daniel Sosah dakika ya 26.

Ni matokeo yanayoiweka katika nafasi ya pili Taifa Stars kwenye Kundi F, baada ya timu ya Taifa ya Algeria kuitwanga Uganda mabao 2-0.

Stars sasa inajiandaa kuikaribisha Algeria katika Uwanja wa Benjamin Mkapa keshokutwa, Jumatano.

Timu mbili zitakazoshika nafasi ya juu katika kila kundi la michuano hiyo, ndizo zitakazofuzu Afcon 2023 nchini Ivory Coast.

## Nabi ataka rekodi Yanga kwa Coastal

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasredine Nabi, ameweka wazi kwamba anahitaji kuweka rekodi ya kipekee kwa kuhakikisha wanafanya vizuri dakika 180 katika michezo miwili ijayo, mmoja wa Ligi Kuu na kisha Fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, dhidi ya Coastal Union ya Tanga.

Yanga inatarajia kucheza mechi ya ligi Juni 15 dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kabla ya kukutana tena na timu hiyo Julai 2, mwaka huu kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA itakayopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anawaheshimu wapinzani wao, Coastal Union na amekiri kuwa wamekuwa bora, jambo ambalo litafanya dakika hizo 180 kuwa ngumu kwa kila upande ila mkakati wake ni kuweka rekodi ya kushinda.

Nabi alisema lengo la kwanza ni kuendeleza kasi yao ya kutafuta matokeo katika mchezo huo na amewataka wachezaji kutambua umuhimu wa mechi hizo kwao binafsi.

Alisema ameona mchezo mzuri na kuwasoma wapinzani wao hao katika nusu fainali ya pili wakati Coastal Union ikicheza dhidi ya Azam FC, hivyo tayari amebaini mapungufu na ubora mkubwa wa wapinzani wao kuelekea mechi mbili wanazokwenda kukutana nao.

"Itakuwa mechi bora na ushindani mkubwa pamoja na ngumu kutoka kwetu kwa sababu wachezaji wa Coastal Union wataingia kwenye mchezo huo wakiwa na ari kubwa," alisema.

"Sina hofu kikubwa ninachokiangalia ni kuhakikisha wachezaji wangu wanafanya kile kitakachotupa matokeo mazuri kwenye michezo yote miwili lengo ni kutovunja rekodi ya kufungwa dakika za mwisho."

Alisema kwa sasa nguvu na akili anazingatia kila mchezo ulio mbele yao kwa kwa kusaka pointi tatu kutoka Coastal Union ambazo wanazihitaji ili kutangaza ubingwa rasmi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunatakiwa kuwa makini hatuwabezi Coastal Union ni wazuri, lakini muhimu zaidi tusipopata alama tatu kwenye ligi basi lazima tukatafute matokeo katika fainali kwa kuwafunga wapinzani hao na kutwaa ubingwa wa ASFC," alisema Nabi.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042